**Neema** zaidi waathirika wa mafuriko Hanang

UKURASA 2&4



**Asakwa** madai kumchoma moto mikono mdogo wake wizi ndizi

UKURASA 7



**TBS** na Polisi kuendesha operesheni magari chakavu

UK. 8



UKURASA 11

ZAYLISA AMEANZA VIZURI 2024


# Nipashe

Jumamosi Januari 6, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581547

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# Vifurushi vipya NHIF vyasitishwa

• **Ni** baada ya mvutano wa wamiliki hospitali binafsi... *Endelea Ukurasa 2*




Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu

## Kipindupindu chaua watano, 452 wawekwa karantini

UKURASA 3

UKURASA 3

## Wafungwa miaka 100 kwa kukutwa na meno ya tembo



**MICHEZO** ENGOLA ASAJILIWA RASMI MSIMBAZI UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Vifurushi vipya NHIF vyasitishwa

**Na Romana Mallya**

BAADA ya kuibuka mvutano kati ya wamiliki wa hospitali binafsi na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuhusu vifurushi vipya vya matibabu, matumizi ya vifurushi hivyo yamesitishwa kwa muda.

NHIF katika taarifa yake jana iliyotolewa na Kaimu Meneja Uhusiano, Grace Michael, ilisema serikali imeunda kamati huru itakayofanya mapitio na kuwasilisha mapendekezo yake serikalini.

Bei mpya zilizotangazwa awali zilipangwa kuanza kutumika Januari Mosi, mwaka huu, lakini kukaibuka sintofahamu baada ya wamiliki wa hospitali binafsi kutishia kusitisha huduma za matibabu kwa wenye kadi za NHIF.

Michael alisema serikali kupitia Wizara ya Afya, juzi ilikutana na watoa huduma kutoka sekta binafsi pamoja na NHIF.

Alisema kikao hicho kililenga kupokea maoni, ushauri na mapendekezo ya kititia cha mafao kinachotarajiwa kuanza kutumika kwa wanachama wake.

"Kutokana na majadiliano katika kikao hicho, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliagiza kuundwa kwa kamati huru itakayofanya mapitio na kuwasilisha mapendekezo yake kwa serikali kabla ya kuanza kutumika. Kamati hiyo inatakiwa kuwasilisha taarifa yake ndani ya mwezi huu.

"Hivyo, mfuko unapenda kuwahakikishia wanachama wake kuwa huduma za matibabu zinaendelea kama kawaida katika vituo vyote vilivyosajiliwa na mfuko na endapo kutakuwa na mabadiliko yoyote taarifa rasmi itatolewa," alisema.

Desemba 18, mwaka jana, NHIF ilifanya mapitio ya kititia cha mafao kwa mwaka 2023, yakilenga kuongeza au kupunguza gharama katika baadhi ya huduma, ili kuendana na bei halisi ya soko.

Baada ya kutangazwa, madaktari bobezi pamoja na wamiliki wa hospitali binafsi waliyalalamikia kwamba hawakushirikishwa katika upangaji wa vifurushi hivyo.

Wengine walioshiriki kikao hicho juzi ni pamoja na wawakilishi wa wamiliki wa hospitali binafsi wakiwamo Tume ya Kikristo ya Huduma za Jamii (CSSC) na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA).

Baadhi ya malalamiko yao yalikuwa kupungua kwa ada ya usajili na ushauri wa daktari katika kititia kipya.

Mabadiliko ya ada ya usajili na ushauri wa daktari viwango ambavyo vilipunguzwa ni kwa wagonjwa kumwona daktari hospitali ya taifa kutoka Sh. 35,000 hadi kufikia Sh. 25,000 kwa daktari bingwa mbobezi na Sh. 25,000 kutoka Sh. 20,000 kwa daktari bingwa.

Pia mabadiliko mengine ni hospitali za rufani za Kanda na kumwona daktari bingwa mbobezi viwango vimepunguzwa kutoka Sh. 35,000 hadi kufikia Sh. 25,000 na kumuona daktari bingwa kutoka Sh. 25,000 na kufikia 20,000.

Hospitali ya mkoa, kumwona daktari bingwa mbobezi kiwango ni Sh. 25,000 kutoka Sh. 15,000 na kwa daktari bingwa ni Sh. 20,000 kutoka Sh. 15,000.

Kwa upande wa kliniki bobezi, kumwona daktari bingwa mbobezi na daktari bingwa kiwango kimepungua kutoka Sh. 15,000 na kufikia Sh. 10,000, huku kwenye kliniki kumwona

# Shehena mafuta ya kula yanaswa bandari bubu

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Kikosi cha Wanamaji katika operesheni zake ukanda wa Bahari ya Hindi, maeneo ya Fungu Yasini, wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, limekamata jahazi likiwa na shehena yenye madumu 1,000 ya lita 20 kila moja ya mafuta ya kupikia ikipelekwa bandari bubu.

Kamanda wa Kikosi cha Polisi Wanamaji, Kamishna Msaidizi (ACP) Moshi Sokoro, alisema jana kuwa operesheni hiyo ilifanyika juzi na kukamata jahazi hiyo iliyokuwa ikitokea Zanzibar kuelekea bandari bubu Kunduchi.

Alisema mafuta hayo yalikuwa katika jahazi liitwalo MV. Huda lenye namba za usajili Z. 2957 lililokuwa likiongozwa na nahodha Mohamed Fumu (36) mkazi wa Bagamoyo, akiwa na wenzake wanne.

"Jahazi hilo lilikuwa na madumu ya mafuya ya kupikia yapatayo 1000 ya lita 20 aina ya Gold Spoon.

"Upelelezi wa awali umeonyesha mzigo huo ulitakiwa kushushawa katika Bandari ya Mbweni ambapo taratibu za kulipa ushuru za forodha zingefanyika lakini badala yake mtuhumiwa huyo alielekea katka bandari bubu ya Kunduchi ili kushusha mzigo," alisema.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na idara nyingine za serikali ili kuhakiki mzigo huo.

Kamanda Sokoro alitoa onyo kwa wafanyabiashara wasio na uadilifu, kufuata taratibu za TRA.



Wakazi wa Mbagala wilayani Temeke jijini Dar es Salaam wakipita kwa taabu kwenye maji baada ya mvua kubwa kunyesha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Neema zaidi waathirika mafuriko Hanang

**Na Halfani Chusi**

WAATHIRIKA wa mafuriko katika wilaya ya Hanang mkoani Manyara, wanatarajiwa kujengewa nyumba na serikali baada ya nyumba zao kuharibiwa na maporomoka ya tope yaliyozoa magogo, mawe na kusababisha hasara kubwa vikiwamo vifo.

Neema hiyo ilitangazwa jana jijini Dar es Salaam na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua zilizochukuliwa kuhusu maafa ya Hanang, Ngorongoro na sekta ya afya.

Alisema mpaka kufikia jana, jumla ya misaada yenye thamani ya Sh. Bilioni 5.2 imetolewa na wadau ikiwa ni pamoja na fedha alizokuja nazo Rais Samia Suluhu Hassan kutoka Dubai.

Matinyi ambaye ni Mkurugenzui wa Idara ya Habari (Maelezo), Alisema maeneo muhimu yatakayoangaliwa katika kuwasaidia waathirika hao ni pamoja na nyumba zilizoathirika na na idadi ya watu huku akisisitiza kuwa tayari serikali imebaini nyumba 89 ziliharibiwa na mafuriko.

"Serikali ilitafuta eneo lililoko kilometa 1.2 kutoka mji mdogo wa Katesh (makao makuu ya wilaya ya Hanang) na mpaka sasa imepima viwanja 269, kati ya hivyo 226 vitakuwa vya makazi, 26 makazi na biashara na 17 huduma za kijamii kama viwanja vya michezo, eneo la maziko, zahanati, eneo la wazi, ofisi ya kitongoji, soko na shule ya msingi moja.

"Hatua inayofuata itakuwa umilikishwaji wa viwanja kwa waathirika ili waanze kujengewa nyumba na nyumba hizo zitakuwa na vyumba vitatu kwa ukamilishwaji na ubunifu wa ramani unaendelea," alisema Matinyi.

Alisema shule tatu zilizokuwa zikitumika kama kambi za waathirika tayari zimeshaandaliwa kwa ajili ya kupokea wanafunzi na uongozi wa wilaya umeshatengeneza ghala lingine ambalo litaendelea kuwa sehemu ya msaada.

"Tathmini mbalimbali zimefanywa Hanang na imethibitika jumla ya ekari 755 za mashamba ya wakulima 366 katika kata sita, ndizo zilizoharibiwa. Serikali imechukua jukumu la kugawa mbegu na mbolea kwa wakulima.

"Kwenye upande wa mifugo iliyopotea, ni ya wafugaji 23 na kati ya hiyo wako mbuzi 115, ng'ombe 70, kondoo 102, nguruwe 12, sungura 15 na kuku 264 ambao thamani yake inakadiriwa kuwa Sh. Milioni 64.9," alisema.

Matinyi alisema kwa mifugo iliyonusurika, serikali inaendelea kugawa chanjo na imejenga majosho 103 na kusisitiza kuwa huduma za urejeshaji maji na uchimbaji visima na umeme imekamilika kwa asilimia 80.

**HABARI KITAIFA**

# Kipindupindu chaua watano, 452 karantini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UGONJWA wa Kipindupindu umetajwa kuibuka katika Kata ya Kagongwa, Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga huku ikielezwa kuwa watu watano wametajwa kufariki dunia na wengine watano kuthibitika kuwa na maradhi hayo.

Wakati hali ikiwa hivyo, wakazi 452 wa eneo hilo wamewekwa chini ya uangalizi wa kitabibu (karantini) katika vituo vya afya maalum vilivyoandaliwa kwa ajili ya kushughulikia wagonjwa hao vya Mwendakulima na Kagongwa. Mkuu wa wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, alithibitisha kuwapo kwa mlipuko wa ugonjwa huo jana wakati akizungumza na vyombo vya Habari. Alisema ugonjwa huo ulianza Desemba 25, mwaka jana, baada ya mtu mmoja kufariki dunia na dalili kuonyesha kuwa chanzo ni ugonjwa huo.

Alisema alipokea taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Mtaa wa Kagongwa kuwapo kwa vifo vya watu watano vilivyoambatana na dalili za kipindupindu ambazo ni kuharisha na kutapika, hivyo kulazimika kutuma timu ya wataalamu kwenda kujua tatizo ni nini. Mhita alisema wataalamu hao walichukua sampuli kwa washukiwa watano wa awali na kwenda kupima ili kupata uhakika na majibu yalitoka na watu hao kubainika kuwa na kipindupindu.

Pia alisema wakazi 452 waliobainika kuwa na dalili hizo, wako chini ya uangalizi wa madaktari wakiendelea na matibabu katika vituo vya afya vya Mwendakulima na Kagongwa, vilivyotengwa kwa ajili ya kuwahudumia.

Alisema hatua zinazoendelea kuchukuliwa kwa sasa ni pamoja na kufunga vilabu vya pombe za kienyeji, kuzuia mikusanyiko isiyokuwa na ulazima na kuendelea kutoa elimu ya kujikinga. Pia aliwataka wananchi kuepuka kula ovyo hasa matunda kwenye maeneo ambayo ni hatarishi bila kuosha hususani maembe.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kagongwa, Michael Shija, alisema Desemba 25, mwaka jana kulitokea kifo cha mtoto aliyekuwa akitapika na kuharisha na wananchi walioshiriki msiba huo, kati yao wawili walizidiwa na siku iliyofuata walifariki dunia kwa dalili hizo hizo.

Pia alisema Januari 2, mwaka huu, alitoa taarifa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama kwa ajili ya kutuma watalaamu wake kuja kuangalia tatizo ni nini baada ya idadi kuongezeka kwa watu wengine wawili kufariki dunia kwa dalili kama hizo.

Alisema watu hao wanne walizikwa na wataalam wa afya huku wengine watano waliobainika kuwa na ugonjwa huo wakiendelea na matibabu na wengine 452 wakiwa chini ya uangalizi wa kitabibu.

Mmoja wa mama lishe, Salome Mabula, alisema elimu aliyopewa na watalaamu wa afya ya namna ya kujikinga na tatizo hilo imemjenga kwa kuweka maji ya moto tiririka ya kunawa na sabuni.

Katika kuhakikisha anatimiza hilo, alisema haruhusu mteja kuingia kwenye mgahawa wake bila kunawa na kuwataka wenzake kuzingatia usafi wawapo kwenye biashara zao.




Mhifadhi wa Ujirani Mwema Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Abed Mwesigwa akizungumza na wakazi wa kijiji cha Machochwe wilaya ya Serengeti juzi na kuwahimiza kutunza mazingira na ushiriki wa uhifadhi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jela miaka 100 kwa kukutwa na meno ya tembo

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MAHAKAMA ya wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza, imewahukumu kifungo cha miaka 100 jela watu watano baada ya kukutwa na makosa matano likiwamo la kukutwa na meno saba ya tembo.

Hukumu ya kesi hiyo ya uhujumu uchumi namba 5/2022, ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mwandamizi Tumsifu Barnabas, huku kila kosa likiwa na kifungo cha miaka 20 kwa makosa yote 20.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Barnabas aliwataja waliohukumiwa kifungo hicho kuwa ni Mkazi wa Ushirombo mkoani Geita, Samson Emmanuel (48), Mkazi wa Itigi mkoani Singida, Shalali Jisandu (40), Hamis Ngurumo (52), Mohammed Nasibu (32) na Mkazi wa Doroto, Mathayo Robert (48).

Hakimu alisema makosa hayo ni kinyume cha kifungu 86(1) na (2) (c) (iii) cha Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori namba 283 ya mwaka 2002 ikisomwa pamoja na aya ya 14 na Kifungu namba 57 (1) na 60(2) cha Sheria ya Kudhibiti Uhalifu wa Kiuchumi namba 200 ya mwaka 2022.

Alisema watu hao walikutwa na hatia ya kukutwa na meno saba ya tembo na silaha ya kivita aina ya G3 baada ya kuridhishwa bila kuacha shaka na ushahidi uliotolewa na mashahidi wa Jamhuri.

"Mahakama baada ya kusikiliza ushahidi wa Jamhuri katika shauri hili, imejiridhisha pasi na shaka kwamba washtakiwa wana hatia na inawahukumu kwenda jela miaka 20 kwa kila kosa na makosa matano yanafanya miaka yao jela kuwa 100 kila mmoja ," alisema Barnabas.

Awali, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Mkaguzi wa Polisi Nyamhanga Mayagi, alisema kwa maeneo tofauti Julai 16,2022, walikutwa na meno saba ya tembo mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 138.9 sawa na Dola za kimarekani 60,000.

Pia alidai kuwa washtakiwa walikutwa na silaha ya kivita aina ya G3 ikiwa na risasi tatu kinyume cha kifungu namba 20(1)(a)(b) na 2 cha Sheria ya Udhibiti wa Silaha na Vilipuzi namba 2 ya mwaka 2015, aya ya 31 na kifungu cha 57(1) na 60(2) cha Sheria ya Kudhibiti Uhalifu wa Kiuchumi namba 200 ya mwaka 2022.

Baada hukumu hiyo wote walichukuliwa mara moja na kupelekwa gerezani kuanza kutumikia kifungo hicho.

# Samia awapa yatima zawadi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa zawadi mbalimbali kikiwamo chakula kwa watoto yatima wanaolelewa katika kituo cha Shinyanga Society For Ophans kilichoko Bushushu Manispaa ya Shinyanga.

Zawadi hizo zilikabidhiwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa, Christina Mndeme, aliyepokea kutoka kwa Rais Samia.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi hizo, Samizi alisema serikali iko bega kwa bega na wadau wa maendeleo ambao wamekuwa wakisaidia makundi maalum kwa kuwapatia huduma ya malezi na elimu.

"Rais Dk. Samia alitoa zawadi hizi kutokana na utaratibu wake wa kila sikukuu kuwashika mkono watoto yatima na wale ambao wanaishi katika mazingira hatarishi ambako kituoni hapa ametoa mchele, sukari, mafuta ya kupikia, nguo na juisi," alisema.

Kwa niaba ya wenzake, Hadija Ally, alimshukuru Rais Dk.Samia kwa kuwapatia zawadi hizo na kuahidi wataendelea kumwombea kwa Mungu ili aendelee kuwa na afya njema ili awatumikie Watanzania na kuwasaidia watoto yatima.

Meneja wa Kituo hicho, Farhiya Said, aliishukuru serikali kwa kuwaunga mkono, huku akiahidi wataendelea kuwapa watoto hao malezi bora pamoja na elimu, na kubainisha kwamba wana watoto 35 na ambao wanasoma shule za msingi ni 26 na sekondari tisa.

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**KELVIN RENATUS LUHALA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 591 AYZ.** Chassis namba **SXA110029624.** Engine namba **3S1940752.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/309/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Bukoba Kituo cha Bukoba Mjini, Mkoa wa Kagera.**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 65/2023**
**Katika Shauri la Mirathi ya Marehemu CHRISTOPHER PAULO KANJAGAILE wa KIBETA – BUKOBA Katika Shauri la Maombi ya Kumteua Msimamizi yaliyoletwa na**
**1. CHRISTIAN R. CHRISTOPHER**
**2. LUCIA K. CHRISTOPHER**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 Mwezi 01 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 22 Mwezi 12 Mwaka 2023.

HAKIMU



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Mkewe Mary Majaliwa wakiwahudumia chakula baadhi ya watoto wa kituo cha kulelea watoto wenye mahitaji maalum cha SWACCO kilichopo wilayani Songea mkoani Ruvuma, wakati wa hafla ya chakula cha mchana aliyoiandaa kwa ajili ya watoto waishio katika kituo hicho jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Majaliwa: Mapambano ukatili ni endelevu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itaendelea na mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili kwa watoto ambavyo husababisha wengi kukimbia familia zao na kukosa makao maalumu.

Kutokana na jitihada hizo za serikali, Majaliwa ameitaka jamii kuendelea kuunga mkono ili kufanikisha azma hiyo.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya chakula cha mchana na watoto wanaolelewa katika makao ya kulelea watoto ya SWACCO, Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Aliwataka maofisa ustawi wa jamii kutekeleza kikamilifu wajibu wao ikiwamo kutambua vituo au makao na kutatua changamoto za ustawi zinazoikabili jamii na kutoa msaada wa kisaikolojia na afya ya akili kwa walengwa.

"Jamii na Watanzania kwa ujumla kila mmoja ashiriki katika kulinda haki na ustawi wa watoto wetu. Hii ni nguvukazi ya taifa letu, hivyo ulinzi na usalama wa watoto ni jukumu letu sote. Mamlaka zinazohusika ziendelee kusimamia, kufuatilia na kuratibu vyema huduma za Makao ya Watoto zinazotolewa na serikali na wadau mbalimbali," alisema.

Waziri Mkuu pia aliutaka uongozi wa mkoa na mamlaka za serikali za mitaa kuweka utaratibu wa kuwatembelea wadau wanaoshirkiana na serikali kutoa huduma kwa wenye uhitaji ili kutambua changamoto walizo nazo na kuzitafutia ufumbuzi, pamoja na kuwapa uelewa kuhusu mipango na mikakati ya Serikali kuhusu huduma za ustawi wa jamii.

Pia aliitaka wizara inayohusika na masuala ya ustawi wa jamii iendelee kushirikiana na wadau kuongeza kasi ya kutoa elimu ya malezi chanya kwa wazazi, walezi na jamii kwa ujumla ili kuwa na nguvu kazi yenye tija kwa taifa.

"Nawashukuru wadau na wafadhili kwa kusimamia makao haya ili kuhakikisha watoto wetu wanapata huduma stahiki za malezi na mahitaji muhimu," alisema.

Katika hatua nyingine, Majaliwa ametoa wito kwa Watanzania wote kuhakikisha watoto wote wenye ulemavu wa aina yoyote, wanapewa fursa ya kupata huduma za jamii ikiwemo elimu waache tabia za kuwaficha ndani badala yake washirikishe mamlaka wakiwamo viongozi wa mitaa, vijiji, kata na wilaya ili kupata msaada.

Majaliwa alisema kuwa suala la kuwahudumia watu wenye ulemavu, kuwapatia vifaa saidizi pamoja na kuhakikisha kuwa wanaguswa moja kwa moja na maendeleo jumuishi, mafanikio yake hayamo katika mikono ya Serikali pekee, hivyo, ni muhimu kwa wadau wote kufanya kazi pamoja ili kuwawezesha watu wenye mahitaji maalum kupata fursa na kuishi bila utegemezi.

Meneja wa kituo hicho, John Chinguku, alisema kituo hicho kilianzishwa Septemba 29, 2000 na Regina Chinguku akiwa na lengo la kusaidia na kuunga mkono jitihada za serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo katika kupunguza changamoto za watoto yatima na wale wanaoishi kwenye mazingira hatarishi kwa kuwapatia huduma za afya, elimu, chakula, mavazi na makazi.

Alisema kituo kilianza kutoa malezi kwa watoto yatima wanne ambao aliwalea kwa kushirikiana na akina mama wengine ambao walikuwa wakijishughulisha na kilimo pamoja na kazi zingine za mikono kwa lengo la kupata mahitaji ya kila siku ya kuwahudumia watoto hao. Kwa sasa kituo kina watoto 50.

Anna Mugenya ambaye ni msaidizi wa mkurugenzi wa kituo hicho, alishukuru serikali kwa ushirikiano inaoutoa katika kituo na hivyo kurahisisha shughuli za uendeshaji yakiwemo malezi kwa watoto. Pia alimshukuru Waziri Mkuu kwa msaada wa vyerehani, vyakula na vifaa vya michezo ya watoto zikiwemo jezi na mipira ambavyo alivikabidhi jana kituoni hapo.

# Kila atakayehama kwa hiari Ngorongoro kulipwa mil. 10/-

**Na Halfani Chusi**

WAFUGAJI wa jamii ya Kimasai waliokubali kuhama Hifadhi ya Ngorongoro kwa hiari kwenda Msomelo, Tanga, wanatarajiwa kulipwa fidia ya Sh. Milioni 10 kwa mali watakazoziacha kutokana na mchakato huo.

Msemaji Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo), Mobhare Matinyi, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam alipokuwa akizungumzia masuala mbalimbali.

Alisema serikali inajenga josho na eneo la malisho, bwawa la kunyweshea mifugo, mnada wa kisasa na vituo vya kupokelea maziwa.

Pia alisema kila atakayehama kupewa nyumba ya vyumba vitatu itakayokuwa katika eneo la hekari mbili na hekari tano za shamba na kwa wenye makaburi kufidiwa.

Akizungumzia kuzorota kwa huduma za kijamii Ngorongoro, Matinyi alisema, "Hakuna sababu ya kuongeza huduma wakati watu wanahama. Jambo la wazi unahamisha watoto wa shule unataka kuongeza shule haiwezekani.

"Tatizo kuna baadhi ya watu na asasi ambazo zinasambaza maneno ya uongo huduma zitaendelea kupanuliwa Msomelo ambako watu wanahamia na sio kule watu wanakohama," alisema.

Kuhusu madai ya baadhi ya hospitali kudaiwa kuwatoza fedha wajawazito alisema: "Ni kweli kuna shida tumekuwa tukizisikia, Wizara ya Afya ina kitengo maalumu kinachofuatilia kila kifo cha mjamzito, pona yao ni pale wananchi watakapomfichia siri.

"Wananchi wasiogope kutoa taarifa, tunapojenga hizi zahanati na vituo vya afya tunataka kuona wanapatiwa huduma kwa kuzingatia weledi."

Hata hivyo alisema katika kipindi cha miaka miwili serikali imeongeza vituo vingi vya afya kutoka vituo 8,549 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 9,366 mwaka 2023, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 9.6, jambo ambalo ni mafanikio makubwa.

Alisema ongezeko hilo, linajumuisha hospitali 436, vituo vya afya 1,126 na zahanati 7,804, sawa na ongezeko la vituo 817 ndani ya miaka miwili.

"Vituo vya afya vya kufanya upasuaji vilikuwa 340 hadi sasa vimefikia 523, sawa na ongezeko la asilimia 25, pia kuna ongezeko la vitanda vya kutolea huduma hali iliyoongeza ufanisi katika huduma ya mama na mtoto.

"Tungependa akina mama wanapokwenda kujifungua wasikabiliwe na tukio la kupoteza watoto lengo letu ni kufikia adhma ya vifo sifuri vitokanavyo na uzazi" alisisitiza.

Alisema vipaumbele vya sekta ya afya ni kuendelea kuimarisha huduma za afya katika mikoa na halmashauri zote nchini.

"Kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, kuongeza watumishi wa afya katika hospitali zote, ninawataka wananchi kutoa taarifa wanapoona hawatendewi haki katika vituo vya afya," alisema.

# Waziri Jafo ataka miradi kukamilika kwa muda uliopangwa

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

MBUNGE wa Kisarawe, Dk. Selemani Jafo, amesema viongozi wanatakiwa kusimamia miradi ya maendeleo kwa kuzingatia kukamilisha miradi kwa wakati na kuondoa vikwazo kwa wananchi.

Amesema katika jimbo hilo mikakati iliyopo ni kila kijiji kuwa na zahanati ifikapo mwaka 2025 ili kuwaondolea adha wananchi wanaotembea umbali mrefu kupata huduma za afya.

Dk. Jafo ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, ameyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wananchi wa vijiji katika kata za Marui, Vikunburu na Chole alipokwenda kukagua miradi ya maendeleo.

Alisema endapo miradi inayopelekwa kwa wananchi viongzi wataisimamia kama ilivyopangwa, itaondoa vikwazo kwa jamii na wataendelea na shughuli zingine za maendeleo na kuinua Uchumi.

Katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa zahanati ngazi ya vijiji, zaidi ya Sh. Milioni 50 zimetolewa kutoka Mfuko wa Jimbo na kwamba ifikapo Machi, mwaka huu, baadhi ya zahanati zitaanza kutoa huduma.

"Nimetembelea miradi ya nyumba ya mwalimu Shule ya Msingi Ngongere na nimeelekeza kupitia fedha za mfuko wa jimbo ikamilike kwa wakati ili hawa walimu wapate sehemu ya kuishi," alisema.

Pia alisema wataalamu wanatakiwa kubadilika na kuzingatia fedha zinazotengwa zinafika kwa wakati maeneo ya miradi ili wanufaika waondokane na vikwazo .

Dk. Jafo alipongeza ujenzi wa Zahanati ya Mafumbi Kata ya Chole ambao alisema uongozi wa kijiji hicho unatakiwa kuigwa kutokana na usimamizi wa miradi pindi wanapopewa fedha.

Katika Jimbo la Kisarawe, kuna vijiji 76 na kati ya hivyo vinane pekee ndivyo havijapata zahanati na hadi sasa kuna vituo vya afya vinane ambavyo vinatoa huduma ikiwamo ya upasuaji .

# Mbegu bora zaongeza uzalishaji alizeti

**Na Elisante John,** SINGIDA

UPATIKANAJI wa mbegu bora ya alizeti kwa bei ya ruzuku, kwa miaka mitatu mfululizo mkoani Singida, umeongeza uzalishaji wa zao hilo kutoka tani 260,382.2 msimu wa 2021/22 hadi zaidi ya tani 400,000 kwa msimu wa mwaka 2023.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa usambazaji wa mbegu za alizeti, zenye ruzuku ya serikali, uliofanyika kwenye viwanja vya Kanisa Katoliki, mjini hapa.

Akitoa salamu kwa mgeni rasmi, Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, Serukamba alisema mafanikio hayo yametokana na serikali kuelekeza nguvu kwenye kilimo kwa kuwapatia wakulima mbegu bora ya alizeti, yenye ruzuku.

Serukamba alisema ili kufikia malengo, mkoa umejiwekea mkakati wa kuongeza uzalishaji wa zao hilo ambao msimu huu wa 2023/24, mkoa unatarajia kulima hekta 323,455.8 kwa ajili ya kuzalisha tani 523,092.5.

"Ili kutekeleza kipaumbele hiki ambacho pia ni mkakati wetu, mkoa unahitaji kupatiwa mbegu bora tani 1,617.3 ambazo tumeziomba kutoka Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) kupitia Wizara ya Kilimo," alisema.

Akizungumza na wakulima, wataalamu wa ugani na viongozi katika uzinduzi huo, Silinde alisema msimu huu, serikali itasambaza nchini mbegu za alizeti tani 2,045, ikijumuisha tani 700 chotara kutoka nje ya nchi na zingine tani 625.4, kutoka kampuni binafsi za ndani ili kuongeza mavuno.

Silinde alisema mkoa wa Singida katika msimu huu utanufaika kwa kupokea tani 600 za mbegu za alizeti ikijumuisha tani 315 chotara za thamani zaidi ya Sh. Bilioni 8.58, sawa na asilimia 42.8 ya mbegu zinazosambazwa nchini.

Naibu Waziri aliupongeza mkoa wa Singida kwa kuongeza uzalishaji wa mbegu na mafuta ya kula ya alizeti msimu uliopita wa 2022/23, kwa kulima eneo lenye ukubwa wa ekari 131,793.3, lililozalisha tani 55,335 za alizeti ghafi, zitakazozalisha lita 1,383,826 ambazo zitapunguza upungufu wa mafuta nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa ASA, Dk. Sophia Kashenge, alisema lengo la wakala ni kumsaidia mkulima kwa kumwezesha mbegu bora ili kufikia malengo aliyojiwekea pia serikali ilivyokusudia kumwinua mkulima nchini.

Dk. Kashenge aliwataka wakulima nchini kutumia mbegu bora hasa zile za uchavushaji huria kutokana na unafuu wa gharama na jinsi ya kuzipata, badala ya zile za chotara, ambazo zinagharimu fedha nyingi kuzipata na hata upatikanaji wake ni wa gharama kubwa.



Mkuu wa mkoa wa Mara, Said Mtanda akihutubia mkutano wa hadhara eneo la Nyatwali, wilayani Bunda juzi na kuwataka wakazi wa eneo hilo kuwa wavumilivu wakati serikali ikijipanga kuwalipa fidia wapishe upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nguvu zaidi kuongezwa utafiti madini

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SERIKALI imebainisha mpango wa kuwekeza katika kufanya utafiti wa kina utakaosaidia kubaini madini yaliyopo nchini na kutafuta njia rahisi za kisasa katika kuchimba ili kuondoa uchimbaji wa kubahatisha.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua kikao cha wizara na watoa huduma kwa wamiliki wa leseni za madini nchini kilicholenga kubaini njia za kuinua sekta hiyo.

Waziri Mavunde alisema licha ya sekta hiyo kufanya vizuri katika ukusanyaji mapato na kuongeza fedha za kigeni nchini, Tanzania ina migodi isiyozidi 10 huku ikiwa na watoa huduma waliosajiliwa zaidi ya 750, hali inayoonyesha kutoridhisha, hivyo kuhitajika uwekezaji mkubwa.

Alisema endapo utafiti wa kina utafanyika na kubaini migodi zaidi, sekta hiyo itakuwa na watoa huduma wa ndani na nje ya nchi wengi zaidi na kuongeza ajira kwa Watanzania na kukuza pato la taifa.

"Dhamira ya serikali ni kuona ushiriki wa Watanzania katika sekta hii unaongezeka maradufu na kuinua uchumi wa kila Mtanzania na taifa kwa ujumla. Pia Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anahitaji kuona sekta hii inakuwa ya mfano kwa manufaa ya nchi nzima," alisema.

Mavunde aliwataka watoa huduma katika sekta hiyo kuungana na kuwa na umoja imara utakaowasaidia kuwa na sauti moja itakayowawezesha kuhudumiwa kwa wakati na serikali.

Pia alitoa wito kwa taasisi za kifedha nchini kuwawezesha kimitaji watoa huduma wenye uhitaji wa kuwekeza ili kuwawezesha kuchangamkia fursa zilizopo katika sekta ya madini nchini.

Awali, akitoa taarifa ya sekta ya madini nchini, Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Mhandisi Yahya Samamba, alisema fursa za ajira katika migodi zimeongezeka kutoka 7,000 kwa mwaka 2018 hadi 16,462 mwaka jana.

"Asilimia 97 ya ajira hizo zimeshikiliwa na Watanzania lengo likiwa ni kutekeleza takwa la serikali la ushiriki wa nchi na wananchi wazawa katika sekta ya madini na bado nafasi hizo kwa wazawa zitaendelea kungezwa kulingana na uhitaji," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, alisema sekta ya madini inachangia kwa kiasi kikubwa pato la mkoa kupitia shughuli mbalimbali zikiwamo usafiri na usafirishaji kwa njia ya ndege.

Alisema serikali itahakikisha ndani ya miezi minane usafirishaji kwa njia ya ndege unaboreshwa kwa asilimia 100 ili kurahisisha usafirishaji wa vipuli na bidhaa nyingine za madini ndani na nje ya nchi.

"Daraja la JPM linaelekea kukamilika ambalo litarahisisha usafirishaji madini kutoka mkoani Geita. Vilevile Mwanza itakuwa na kituo kikuu cha reli ya kisasa (SGR) pamoja na bandari kavu ya Fela. Hii itakuwa furusa kubwa kwa wafanyabiashara wa madini na sekta zingine," alisema Makalla.

Makalla alilitaka Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kujihakikishia uwezo wake wa kuhudumia wafanyabiashara mkoani Mwanza ikiwa ni pamoja na kuimarisha usafirishaji mizigo pindi ukarabati wa uwanja huo utakapokamilika ili kutokukwamisha shughuli za kiuchumi na kuwataka kuruhusu uwekezaji pindi itakapohitajika.

Mmoja wa watoa huduma katika sekta hiyo, Mhandisi Francis Labana, aliiomba serikali kusimamia mazingira ya kampuni za wazawa zilizoungana kukubalika kufanya uwekezaji katika migodi mikubwa ili kuinua teknolojia na kuboresha upatikanaji wa ajira kwa Watanzania.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Nyota Taifa Stars msiogope majina ya wapinzani AFCON

**TIMU** ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika maarufu AFCON ambazo mwaka huu zitafanyika kuanzia Januari 13 hadi Februari 11 nchini Ivory Coast.

Hii ni mara ya tatu kwa Tanzania kushiriki mashindano hayo makubwa kwa ngazi ya timu za taifa hapa barani Afrika, mara ya kwanza ilikuwa ni mwaka 1980 michuano ilipofanyika Nigeria na ilifuzu kwa mara ya pili kushiriki fainali zilizochezwa Misri mwaka 2019.

Wakati Taifa Stars ikifuzu kwa mara ya tatu, dada zao (Twiga Stars), pia wamekata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON), wao wakienda katika mashindano hayo kwa mara ya pili, mara ya kwanza walishiriki fainali zilizofanyika mwaka 2010 huko Afrika Kusini, kikosi kikiwa chini ya Boniface Mkwasa.

Ni jambo la kujivunia kwa timu zote mbili kufuzu fainali hizo, tena zikiwa ndio timu pekee kutoka katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Tunapenda kutoa pongezi kwa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wachezaji na wote waliosaidia kuzifikisha timu hizo hapo bila kusahau mashabiki ambao walihudhuria michezo yote ya nyumbani na ugenini wakati wawakilishi wetu wakipeperusha bendera ya nchi.

Zikiwa zimebakia siku sita kuanza kwa fainali hizo, kikosi cha Stars kinachonolewa na Kocha Mkuu, Adel Amrouche, anayesaidiana na Hemed Suleiman Morocco, kinaendelea na maandalizi ya kuhakikisha wanakuwa imara katika kambi maalumu iliyoko Misri.

Taarifa rasmi kutoka TFF zinasema Stars itacheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya wenyeji The Pharaos keshokutwa na baada ya mechi hiyo itaelekea Ivory Coast.

Tunafahamu Stars ilitakiwa kujiimarisha tangu pale ilipokata rasmi tiketi ya kushiriki fainali hizo na pale ilipowafahamu wapinzani wake walioko katika Kundi F ambao ni Morocco, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Tulizoea kusema "Stars yapangwa kundi la kifo" na vichwa vingine 'vigumu' vya habari kuonyesha Tanzania inaenda kusindikiza na si kushindana, kauli hii imepitwa na wakati kwa sababu sasa hivi Tanzania inaingia katika fainali hizo ikiwa na wachezaji mchanganyiko.

Stars ya sasa si ile ya miaka ya nyuma ambayo ilikuwa inaingia katika mechi kubwa bila ya wachezaji wanaocheza soka la kulipwa, kikosi kinachotarajiwa kwenda AFCON ijayo kinaundwa na mchanganyiko wa wachezaji wanaocheza ligi za nchi mbalimbali ambao wameiongezea nguvu timu hiyo.

Katika dunia ya sasa, hakuna timu kubwa au ndogo, tukumbuke katika soka lolote linaweza kutokea endapo wachezaji wataongeza umakini na utulivu wanapokuwa na mpira.

Kwa misingi hiyo, wachezaji wa Stars wanatakiwa kuingia dimbani kucheza mechi kwa kujiamini na lolote linaweza kutokea kama ambavyo nahodha, Mbwana Samatta, alivyosema muda mchache baada ya kuungana na wachezaji wenzake huko Misri.

Ni kweli Morocco, Zambia na DRC ni nchi ambazo zimeshawahi kubeba taji la Afrika, lakini kama ambavyo mataifa hayo yalianza, Stars pia inaweza kujifungulia ukurasa wake mpya kwa kupambana na hatimaye kupata ushindi utakaoifanya isonge mbele na si kuishia hatua ya makundi.

Lakini tukumbuke wakati tunaendelea kujiimarisha kufanya vyema katika fainali hizi, tutumie michuano hii kama 'darasa' kuelekea mechi za kufuzu fainali za Kombe la Dunia ambazo ziko mbele yetu.


Wachezaji wa Stars waende katika fainali hizo wakijiamini na wanaweza kuweka rekodi mpya kama iliyowekwa na Serengeti Girls ambayo ilishiriki kwa mara ya kwanza Fainali za Kombe la Dunia na kutinga hatua ya robo fainali, hilo linawezekana kama kila mmoja atatimiza vyema majukumu yake.

**Kila la kheri Taifa Stars, kila la kheri Tanzania.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mastaa kutemwa Stars kawaida, kocha aachwe afanye kazi yake

Na Adam Fungamwango

**KUMEZUKA** mjadala mkubwa juu ya kuachwa kwa baadhi ya wachezaji katika kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars).

Mara baada ya kundi la mwisho la wachezaji 25 watakaokwenda kucheza Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), zinazotarajiwa kufanyika kuanzia Jumamosi ijayo nchini Ivory Coast, ikazuka mijadala mbalimbali katika mitandao ya kijamii, redioni, televisheni na hata mitaani, juu ya uamuzi wa Kocha Mkuu, Adel Amrouche, kuacha baadhi ya nyota.

Wachezaji ambao Watanzania wengi wameonekana kama hawakuridhika kuachwa ni pamoja na Kelvin John maarufu Mbappe anayesakata soka la kulipwa katika klabu ya Genk iliyoko Ubelgiji na Clement Mzize wa Yanga.

Amrouche akalazimika kutoa ufafanuzi kwa nini amemwacha Kelvin, kocha huyo alisema nidhamu ndiyo imemwondoa na si uwezo wake uwanjani.

Aliongea mengi juu ya mchezaji huyo na wakati mwingine aliongea kama kocha na baadaye akazungumza kama mzazi.

Hakutaka kufafanua ni utovu gani wa nidhamu kwa sababu alisema akiweka hadharani inaweza kumwathiri kiasi cha kushindwa kukitumikia vyema kipaji chake.

Nadhani sidhani tena kama kuna shabiki anayeutakia mema mpira wa Tanzania na mchezaji mwenyewe anaweza akaendelea kuuliza ni kitu gani alichokifanya.

Sisi wengine wenye kujiongeza tumeshajua na yaishie hapo hapo, waswahili wana msemo wao fulani 'yasiende kwa jumbe.'

Wengine tumeshamwelewa kwa hiyo inabaki kama ilivyo, lakini hakufafanua kwa Mzize ambaye sasa amejiunga katika kikosi cha Yanga kinachoshiriki mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

Nadhani ni kuwapo kwa wachezaji wengi kwenye eneo hilo ambao ni wazoefu kuliko yeye, akiwamo nahodha, Mbwana Samatta.

Katika michuano kama hii ambayo haina mechi nyingi, huwezi kuchukua wachezaji kama watatu au pungufu ya hapo katika namba moja.

Ikumbukwe awali waliitwa wachezaji 53, hivyo ni lazima wengine waachwe ili wapatikane 25 wanaotakiwa kwenda kuiwakilisha nchi.

Niwakumbushe tu mashabiki wa soka Tanzania, Amrouche si kocha wa kwanza kuacha wachezaji ambao Wabongo walitaka waende kuitumikia Stars, mwaka 2019, aliyekuwa Kocha Mkuu wa Stars, Emmanuel Amunike, aliwachuja wachezaji kadhaa akiwamo Jonas Mkude, Shomari Kapombe, Ibrahim Ajibu, Kennedy Juma, Ally Ally, Ayoub Lyanga na Khamis Kassim kutoka Kagera Sugar.

Majina yaliyotikisa vyombo vya habari wakati huo, huku mashabiki wakichrumba kwa nini wameachwa ni Mkude na Ajibu.

Ajibu, wakati huo anatemwa Stars, Ajibu alikuwa ndio kinara wa pasi za mabao maarufu mama 'assist', huku Mkude akiwa kiwango bora mpaka kuisaidia Simba kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hapa kilichoonekana kulikuwa na Usimba na Uyanga, lakini pamoja na mapenzi binafsi kwa baadhi ya wachezaji.

Wengine hawakupigiwa kelele wala kutetewa, lakini Amunike akabaki na msimamo wake hadi mwisho.

Mashabiki wa Tanzania sasa wabadilike na kujenga utamaduni wa kumwachia kocha kufanya kazi yake.

Anapochagua wachezaji ni yeye mwenyewe anaona ndiyo wanaomfaa na anapokuwa nao katika mazoezi anaona wale ambao wataenda kumpa mafanikio katika michuano husika.

Hakuna kocha anayetaka kufungwa duniani, kwa hiyo anafanya hivyo kwa nia njema tu na kama timu ikifanya vibaya ni yeye ndiye anayepoteza kibarua na wala si mashabiki.

Ameshafanya hivyo, na yeye ndiye aliyepewa jukumu hilo kama mtaalam, tumwache afanye kazi yake, Wabongo kazi yetu iliyobaki ni kuishangilia tu.

**Kila la kheri Taifa Stars katika fainali za AFCON.**

HABARI KITAIFA

# Raia wa Tanzania, Burundi kizimbani madai ya kughushi

**Na Grace Gurisha**

RAIA wawili wa Burundi na Watanzania watatu wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wakikabiliwa na mashtaka matatu likiwemo la kutumia kibali cha kuishi nchini cha kughushi na kubadili maudhui ya kibali hicho.

Washtakiwa hao ni Gretta Akimana na Japhet Hagabimana ambao ni raia wa Burundi na Danleeh Nyirenda, Peter Mchuno na Francis Lukanina (Watanzania) na ambapo walifikishwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Romuli Mbuya.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali kutoka Idara ya Uhamiaji, Khadija Masoud, alidai kuwa watu hao wanashtakiwa kwa mashitaka matatu ambayo waliyatenda Desemba, mwaka jana, ndani ya mkoa wa Dar es Salaam.

Alidai kuwa katika shtaka la kwanza linamkabili Akimana peke yake, Desemba 22, 2023 katika Ofisi za Uhamiaji, Kurasini, Temeke mkoani Dar es Salaam, alikutwa akitumia kibali cha kuishi nchini kilichoghushiwa huku akijua ni kinyume cha sheria.

Katika mashtaka mengine ya kubadili maudhui ya hati hiyo yanayowakabili washitakiwa wote watano, ilidaiwa kuwa Desemba 22, 2023 katika eneo hilo, mshtakiwa Akimana na wenzake wanne walikutwa wakiwa wamebadili maudhui ya hati ya ukaaji yenye jina la Gretta Akimana.

Ilidaiwa kuwa walibadili maudhui hayo wakionesha kuwa hati hiyo imetolewa na mamlaka husika huku wakijua kuwa si kweli.

Katika shitaka la kumsaidia mtu kutenda kosa, Nyirenda, Mchuno na Lukanina wanadaiwa wakiwa katika eneo hilo, walikutwa wakiwa wamemsaidia mshtakiwa wa kwanza (Akimana) kughushi kibali cha makazi huku wakiwa wanajua kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

Baada ya washtakiwa kusomewa mashitaka hayo, walikana kuhusika na Hakimu Mbuya alisema dhamana kwa washtakiwa iko wazi na kila mshtakiwa atatia sani bondi ya Sh. 750,000 na mdhamini mmoja mwenye makazi ya kudumu mkoani Dar es Salaam ambaye pia atatia saini bondi ya Sh. 750,000.

Mshtakiwa namba tatu (Nyiremba) ndiye aliyetimiza masharti hayo ya dhamana na kuachiwa na wengine walipelekwa rumande hadi watakapokamilisha masharti hayo.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Januari 19, mwaka huu kwa ajili ya kusoma hoja za awali.



Wananchi wakishiriki ujenzi wa sekondari ya wasichana ya masomo ya sayansi mkoa wa Mara, inayojengwa eneo la Bulamba jimbo la Mwibara juzi. Kwa sasa serikali inajenga sekondari za aina hiyo kila mkoa ikiwa ni njia ya kuwahamasisha wanafunzi kusoma masomo hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Asakwa madai kumchoma moto mikono mdogo wake

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linamsaka, mwanafunzi wa kidato cha tano, Zedekia Maguchi (18), mkazi wa Halmashauri ya Mji Njombe, Mkoa wa Njombe, kwa tuhuma za kumchoma moto mikono mdogo wake Rose Sagauli (7).

Tukio hilo limetokea Jumatano ya wiki hii, majira ya saa 12 asubuhi katika Kitongoji cha Msete mjini hapa.

Akizingumza na mwandishi wa habari hizi jana kwa njia ya simu, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Butusyo Mwambelo, alisema wakati tukio hilo likitokea mama yao alikuwa amekwenda kanisani.

"Huyo binti ambaye ni mwanafunzi wa awali alichukua ndizi mbili zilizoiva akala, kaka mtu hakuridhika akamshika mikono akamuweka kwenye moto wa kuni, kwa hiyo mama yake wakati anarudi akakuta mtoto wake kaungua ikabidi ambebe kumpeleka hospitalini," alisema Mwambelo.

Kaimu Kamanda alisema mara baada ya Zedekia kufanya tukio hilo alikimbilia na jitihada za kumtafuta zinaendelea.

"Tunafanya jitihada za kumkamata kwa sababu ni mwanafunzi kwa hiyo, inawezekana baada ya kuona mdogo wake ameungua akakimbia.

"Kwa hiyo, tunaendelea kufuatilia atakuwapo tu hata shule hawezi kwenda kwa sababu mama mzazi yuko hospitalini na fedha iliyotakiwa kumsaidia ndiyo hiyo imeenda kumtibia mtoto," alisema.

Kutokana na tukio hilo, Mwambelo alitoa wito kwa wazazi kuwapa elimu watoto wao na kuwafundisha maadili mazuri, kwa sababu mtoto huyo bado ni mdogo, lakini anaroho ya kikatili.

"Mtoto kuwa na roho hiyo atakuwa ni mtu mbaya kwenye jamii, kwa hiyo sisi wazazi tunajukumu la kukaa na watoto wetu, kila wakati na kila siku tuwaase wawe na maadili, wawe na hofu ya Mungu, kwa sababu huyo ni mdogo wake tumbo moja, lakini amemfanyia ukatili," alisema Mwambelo.

Awali, Mwenyekiti wa Mtaa wa Mji Mwema, Leonard Mkupi, alisema inadaiwa kuwa, sababu ya mtoto huyo kuchomwa moto ni mara baada ya kuhisi njaa na kuingia ndani kuchukua ndizi mbili na kula.

"Kaka yake huyu Zedekia akamkamata na kumfunga mikono yote miwili na akawasha jiko la kuni na kumchoma moto mikono," alisema Mkupi

# Taasisi za umma, binafsi zahimizwa ukuzaji uchumi

**Na Sabato Kasika**

TAASISI za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na binafsi zimehimizwa kuendelea kushirikiana katika kutangaza kazi zao, ili kusaidia kukuza uchumi, na kuinua kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Makamu wa Pili wa Rais Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, aliyasema hayo katika maonyesho ya maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Maonyesho hayo ya kutangaza shughuli za maendeleo, yalifanyika Mnara wa Kumbukumbu ya Mapinduzi Kisonge, Unguja juzi ambapo kiongozi huyo alisema, ni jambo muhimu kwa taasisi hizo kutangaza kazi kwa pamoja.

"Maonyesho haya ya kutangaza kazi zenu kwa pamoja yaendelezwe, kwani wananchi wanapata fursa kufahamu bidhaa au huduma zinazofanywa na sekta husika. Ninaomba Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuendelea kufanya hivyo," alisema Balozi Idd.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema lengo la maonyesho hayo ni kuwapa mwamko wananchi kujituma ili iwe chachu ya kujenga taifa na kuakisi malengo ya waasisi wa Mapinduzi.

"Ili kujenga msingi wa heshima na utu wa mwanadamu, ipo haja ya kufanya kazi kwa kushirikiana na kubadilishana uzoefu na taasisi zilizoshiriki maonyesho hayo, kwani itasaidia kuleta umoja wa Wazanzibar katika kujikomboa kutoka katika umaskini," alisema Soraga.

Alisema, Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji imeona ipo haja ya kushirikisha taasisi hizo kujitangaza kupitia maonyesho hayo, wananchi wafahamu namna ya kupata huduma zinazotolewa.

Mmoja wa washiriki wa maonyesho hayo, Amina Said Ali, alipongeza Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kuandaa maonyesho hayo.

Maonyesho hayo ya huduma na bidhaa yameshirikisha zaidi ya taasisi 50 za umma na binafsi.

# Umwonapo popote tao taarifa haraka



Na Sabato Kasika

GABRIEL Msagala (20) (pichani) mwenye tatizo la akili, anatafutwa na ndugu zake baada ya kutoweka nyumbani Makongo juu, jijini Dar es Salaam na kwenda kusikojulikana.

Akizungumza katika ofisi za gazeti hili Mikocheni Dar es Salaam jana, shangazi yake, Angella Benard, alisema, Gabriel alitoweka Januari 3 majira ya saa tisa alasiri.

"Tumetoa taarifa katika kituo cha polisi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kufungua jalada namba CHD/RB/25/2024. Tunaomba atakayemuona popote atoe taarifa kituo chochote cha polisi," alisema Angella.

Aidha, Angella alisema, mtu yeyote ambaye atamuona kijana huyo, anaweza kuwasiliana naye (Angella) kwa simu namba 0673-878738 au 0754-608798.

"Gabriel nyumbani kwao ni KIjiji cha Mwandi, wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, alikuja Dar es Salaam wiki tatu zilizopita, akiwa ametoroka kutoka huko na sasa ametoroka tena," alisema.

# TBS, Polisi kuendesha operesheni magari chakavu

Na Joseph Mwendapole

JESHI la Polisi kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), wametia saini makubaliano ya kufanya operesheni kabambe ya ukaguzi wa magari nchi nzima ili kuyabaini na kisha kuyaondoa barabarani yale ambayo yataonekana hayafai kwa matumizi.

Ukaguzi huo utaanza hivi karibuni kwa kutumia mitambo na vifaa vya kisasa vya TBS ikiwa ni hatua ya kupunguza ajali za barabarani ambazo kwa mujibu wa Jeshi la Polisi, mara nyingi husababishwa na ubovu wa baadhi ya magari.

Makubaliano hayo yalitiwa saini jana baina ya Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athumani Ngenya na Kamishna wa Mafunzo na Operesheni wa Jeshi la Polisi, Awadh Juma Haji, kwenye ukumbi wa Polisi, Osterbay, Dar es Salaam. Akizungumza baada ya kutia saini makubaliano hayo, Kamishna Awadh alisema lengo ni kuhakikisha vyombo vyote vya moto vinakaguliwa na kuwa katika ubora unaotakiwa ili kupunguza ajali.

"Ili vyombo vya moto viwe bora lazima vikaguliwe na vyombo vya kisasa tofauti na zamani ambapo tulitumia vifaa vya kawaida tofauti na hivi ambavyo tutaanza kuvitumia baada ya kuingia kwenye makubaliano na wenzetu TBS ambao wana vifaa na mitambo ya kisasa zaidi tuhakikishe watumiaji wa barabara wanaendelea kuwa salama," alisema.

Kamishna Awadh alisema ukaguzi huo utaanza kwa awamu katika kanda sita nchini kama sehemu ya majaribio na watakwenda kwenye mikoa yote kuendesha operesheni hiyo kuhakikisha magari yote yanafikiwa na yanaangaliwa ubora wake.

Alisema kwa mujibu wa sheria, magari binafsi yanatakiwa kukaguliwa mara moja kwa mwaka wakati magari ya biashara kama mabasi na yale ya kusafirisha wanafunzi, yanatakiwa yawe yanafanyiwa ukaguzi mara mbili kila mwaka.

"Mmiliki wa gari atakapopeleka gari lake kwenye kituo cha ukaguzi na likikaguliwa atapatiwa cheti cha ukaguzi na baada ya muda uliowekwa kisheria kama ni miezi sita au mwaka mmoja, mmiliki atawajibika kurudi tena kufanyiwa ukaguzi huo wa lazima tena na kupewa cheti hicho, nawaomba wamiliki wote wa magari watii agizo hili ambalo liko kisheria," alisema.

Alisema barabarani kuna ajali zinazosababishwa na makosa ya kibinadamu lakini ajali zingine zinatokana na ubovu wa magari na ndiyo sababu wamedhamiria kuanza kufanya ukaguzi wa ubora wa magari kwa kutumia vifaa na mitambo ya kisasa zaidi.

Kamishn Awadhi aliahidi kuwa Jeshi la Polisi litatoa ushirikiano wote unaotakiwa kwa TBS kuhakikisha malengo yote yaliyokusudiwa yanafikiwa kwa magari yasiyo na ubora kutoendelea kuwa barabarani.

Katika hatua nyingine, Awadhi aliwaonya wenye magari ambao wamekuwa na kawaida ya kuweka vioo vya giza kwenye taa na kwenye vioo vya mbele hali ambayo alisema inasababisha uoni hafivu na kuhatarisha usalama barabarani.

"Kioo cha mbele kikiwekewa giza kinasababisha uoni hafifu na taa pia zinapowekewa giza zinakuwa hafifu na kuhatarisha usalama wa barabarani kwa hiyo nawaonya wote watakaokamatwa na kuwachukuliwa hatua kali na wasitulaumu tutakapoanza kuwakamata," alisema

Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya, alisema ajali nyingi za barabara zinasababishwa na uzembe wa madereva na wakati mwingine ubovu wa barabara ndiyo sababu wameamua kuanza ukaguzi wa aina hiyo kuhakikisha magari yote yanakuwa na ubora.

"Polisi wamekuwa wakifanya ukaguzi kwa njia za kawaida lakini sisi TBS tuna utaalamu na vifaa vya kisasa vya kukagua magari sasa tulipozungumza na kuonekana tunauwezo huo ndipo tukaona tuingine kwenye makubaliano kama haya ambayo tumeingia leo," alisema




Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Magomeni, Mary Marungi akibofya kitufe kuchezesha droo ya wiki ya tisa ya kampeni ya kuhamasisha matumizi yasiyo ya pesa taslim 'NMB MastaBata Halipoi' kumtafuta mmoja wa washindi wa droo hiyo, ambapo washindi 100 walijishindia shilingi milioni 10. Kushoto ni Mkaguzi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Rasuli Masoud pamoja na Meneja Huduma za Kadi, Ednamamu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vituo viwili kupozea umeme kujengwa Geita

Na Mohab Dominick,
MBOGWE

SERIKALI imesema itajenga vituo viwili vidogo Nyakanazi na Kahama kwa ajili ya kupozea umeme ili kuhakikisha Wilaya za Bukombe na Mbogwe mkoani Geita zinakuwa na nishati ya umeme wa kudumu na uhakika wakati wote.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, aliyasema hayo juzi wakati akiongea na wananchi wa Wilaya ya Mbonge.

Alisema kama kituo kidogo cha kupoozea umeme kitakuwa Nyakanazi, hivyo Wilaya za Bukombe na Mbonge zitapata nishati ya umeme kwa urahisi zaidi.

Dk. Biteko alisema wilaya nyingi hazina vituo vya kupoozea umeme na ndio maana serikali imeamua kufungua kituo hicho katika kata ya Nyakanazi wilayani Biharamulo ili wilaya hizo ziweze kunufaika.

Naibu Waziri Mkuu huyo alisema serikali pia, inatarajia kujenga kituo kingine kama hicho wilayani Kahama ambacho kitasaidia changamoto ya umeme katika maeneo hayo.

Alisema uwapo wa vituo vitatu vya kupoozea umeme utasaidia kwa kiasi kikubwa katika kukuza uchumi wa maeneo hayo na kuchochea mabadiliko ya kiuchumi.

"Katika wilaya za Mbonge na Bukombe hakuna kituo hata kimoja cha kupoozea umeme, umeme unatoka katika Kata ya Kakola, Wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, ambako ni mbali na hata kukitokea hitilafu siyo rahisi kuelewa ni sehemu gani.

"Tumeamua kujenga vituo vidogo vingine katika maeneo ya Nyakanazi pamoja na Kahama ambako ni karibu zaidi," alisema Biteko.

Mbunge wa Mbogwe, Nicodemus Maganga, aliwataka wananchi kuwa wavumilivu kwa kuwa mchakato wa kupata nishati hiyo unaendelea.



## HABARI DODOMA

# RC atangaza adhabu wachelewaji shuleni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema mtoto yeyote atakayechelewa kuripoti shule kwa wakati bila sababu za msingi atapewa adhabu ya kulima matuta 10.

Senyamule alisema hayo jana akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua miradi ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Michese, kusikiliza na kutatua kero za wananchi katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

"Wazazi msiwasababishie watoto adhabu ya kulima matuta 10 kwa sababu ya kuchelewa kufika shule kwa wakati na kuchelewa kuanza masomo. Wanafunzi wanaanza kusoma tangu siku ya kwanza wanapofungua shule.

"Dodoma tunataka ufaulu wa kiwango cha juu kama ilivyo hadhi ya makao makuu ya nchi yetu. Tunaendelea kufanya vizuri kwenye masomo na hatutaki kurudi nyuma," alisema.

Senyamule alikagua ujenzi wa shule hiyo katika kata ya Mkonze eneo la Michese na kuagiza kukamilika kwa ujenzi ili ifikapo Januari 08, mwaka huu ili wanafunzi wakae kwenye madarasa yenye ubora.

Alisema anahitaji kuona ujenzi huo unakamilika kwa wakati ili yaanze kutumiwa na wahusika katika utoaji elimu.

Kaimu Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dodoma, Justin Machela, alisema wazazi wanapaswa kuwapeleka watoto shuleni ili kuhakikisha wanaanza masomo kwa wakati na kuwanunulia vifaa vinavyohitajika shule ikiwemo madaftari na kalamu.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Michese, Andrew Rumishaeli, alisema shule hiyo ilipokea Sh. milioni 544 zikiwa ni fedha za mradi wa SEQUIP kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vinane vya madarasa vyenye ofisi mbili, jengo la utawala, jengo la maktaba, jengo la teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), vyoo vya wanafunzi matundu manane, kichomea taka na tangi la maji la ardhini.

# Mtaalamu aonya athari matumizi ya simu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KUZUNGUMZA na simu kwa muda mrefu pamoja na kufanya kazi katika mazingira yenye kelele, kunachangia kwa kiasi kikubwa upotevu wa usikivu, imeelezwa.

Leonard Tibihika, mtaalamu wa upimaji usikivu katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) alibainisha hayo jana kwenye mahojiano maalumu kuhusu huduma za uchunguzi wa usikivu hospitalini hapo.

"Isitafsirike vibaya si kila anayeongea na simu anahatarisha usikivu, bali yule anayetumia muda mrefu kuongea na simu kwa sababu mgandamizo wa mawimbi ya sauti inayoingia sikioni ukiendelea kwa muda mrefu, huathiri ngoma ya sikio" alisema Tibihika.

Alisema watu wengine walioko katika hatari ya kupoteza usikivu ni wale wanaofanya kazi katika mazingira ya kelele, wafanyakazi wa viwandani, wanaokesha kwenye klabu za muziki, na wale wenye shughuli katika masoko.

Madhara anayoweza kukutana nayo, alisema ni kutogundua mapema kuwa usikivu wake hauko katika kiwango cha kawaida na kuchukua hatua kwa sababu usikivu huanza kupungua polepole hadi atakapoambiwa na wengine.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, kuchelewa kugundua kuwa usikivu unapotea au kugundua na kutochukua hatua za kuchunguzwa ili kutibiwa, husababisha watu wengi kufika hospitalini wakiwa katika hatua mbaya kiasi ambacho inaweza kuhatarisha kupoteza usikivu kabisa.

"Taarifa za vituo vya Udhibiti na Kukinga Magonjwa (CDC) zinadokeza kuwa watoto na vijana wadogo milioni 5.2 na watu wazima milioni 26 hupoteza uwezo wa kusikia kutokana na kuwa kwenye mazingira ya kelele," alisema.

Alisema moja ya utafiti kuhusu kupoteza usikivu kwa matumizi makubwa ya simu uliobandikwa katika tovuti ya Shirika la Afya Duniani (WHO), unathibitisha kuwa matumizi ya zaidi ya dakika 60 kila siku yanaweza kuathiri usikivu wa binadamu ndani ya miaka mitano.

Kutokana na athari hizo, alitoa wito kwa watumiaji wa simu kwa muda mrefu kuchukua hatua za kujikinga pamoja na kuhakikisha wanafanyiwa uchunguzi wa usikivu angalau mara mbili ndani ya miezi 12.

Benjamin Mkapa, ni miongoni mwa hospitali tatu za serikali nchini zinazotoa huduma za uchunguzi wa usikivu kwa kufanya vipimo vya aina zote na asilimia kubwa ya wagonjwa wanaopoteza usikivu hubainika wakiwa na tatizo la kupasuka ngoma ya sikio.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule ( wa tatu kutoka kushoto) akikagua ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Michese, inayojengwa kata ya Mkonze katika Jiji la Dodoma jana, wengine kutoka kushoto ni Kaimu Ofisa Elimu wa Sekondari Jiji, Nicodemous Kileo na Mhandisi wa Jiji la Dodoma, Fredy Mwakisambwe. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Jiji lapiga marufuku ushushaji holela mizigo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imepiga marufuku kushusha mizigo katika maeneo yasiyoruhusiwa yakiwamo masoko huku ikionya kuwa watakaobainika hatua za kisheria zitachukuliwa.

Marufuku hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Kaimu Mkurugenzi wa Jiji, Joseph Fungo, baada ya kufanya msako na kuyakamata malori 11 yaliyokuwa yakishusha matunda, nazi, ndizi na viazi kwenye soko la sabasaba ambalo limezuiwa kushusha mizigo hiyo.

Fungo aliwaambia waandishi wa habari kuwa halmashauri itaendelea kuyakamata malori yanayokiuka maelekezo ya kushusha mizigo yao.

Alisema halmashauri imetoa maelekezo malori yote yanayoingiza matunda yashushe soko la Ndugai na si sabasaba, hivyo kwa hayo yaliyokamatwa lazima walipishwe faini au kuburuzwa mahakamani.

"Magari hayo yaliyoondolewa namba za magari eneo la soko la Sabasaba ni jambo ambalo limefanyika kisheria kabisa kwa sababu tulishapiga marufuku magari yote yanayoleta bidhaa iwe ya matunda, ndizi, nazi na viazi yashushie soko la Ndugai na si vinginevyo na watakaokaidi tutapelekana kwenye vyombo vya kisheria," alisema.

Fungo alisisitiza kwa kutoa tahadhari kwa wafanyabiashara ambao wanafanya kwenye maeneo yasiyo ruhusiwa kuwa wakikamatwa watalazimika kupelekwa kwenye vyombo vya sheria ikiwamo mahakamani kwa hatua zaidi.

Alisema maeneo ya kufanyia biashara yapo na tayari yameshatengwa yakiwamo soko la Machinga, Bonanza, Majengo, Kikuyu, Kisasa, Chadulu na Chang'ombe na mengineyo yaliyoko kwenye kata zilizoko ndani ya jiji. Mmoja wa madereva wa malori hayo, Salum Athuma , alisema wanachofahamu kushusha mizigo kwenye masoko yaliyoko katikati ya jiji mwisho ni saa 4:00 asubuhi, hivyo wanashangaa kuona wanakamtwa.

"Kwetu sisi tunafikiri huu mradi wa kuyakamata magari yetu tunayoleta mizigo ya matunda unatengenezwa na wakubwa walioko jiji ili tuwapatie fedha za rushwa. Tunasema hivyo kutokana na ukweli kwamba kwa muda mrefu tumekuwa tukishusha mizigo kwenye masoko ya Majengo, Sabasaba na Chang'ombe," alisema.





## Waagizwa kurekebisha dosari kukinga majanga

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Uendeshaji na Huduma za Kibinadamu kutoka Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, Haji Faki Hamduni, amewataka wamiliki wa hoteli kurekebisha upungufu uliopo ili kujikinga na maafa.

Aliyasema hayo jana Maruhubi baada ya kufanya ukaguzi katika Hoteli ya Zanzibar Ocean View Kilimani, wilaya ya Mjini.

Alisema katika ukaguzi huo kumeonekana baadhi ya kasoro, hivyo kuna haja ya kurekebisha mapema ili kuondosha athari zinazoweza kujitokeza.

Haji alisema kuwa lengo la kufanya ukaguzi huo ni kuangalia usalama na viashiria vinavyosababisha maafa na kufanya marekebisho kabla maafa kutokea.

Alisema wameamua kufanya hivyo ili kutekeleza matakwa ya sheria ya kufanya ukaguzi katika taasisi zote za serikali na binafsi na kutoa miongozo inayofaa.

Pia alisema wameamua kwenda katika hoteli hiyo kutokana na kuwapo baadhi ya viashiria hatarishi ikiwamo miti pembezoni mwa hoteli.

Iwapo watagundua viashiria vyovyote, alisema hawatasita kutoa maagizo na kufanyiwa kazi kwa muda uliotolewa na endapo watashindwa kufanya marekebisho, kamisheni itachukuwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Sisi tunatoa maagizo kutokana na mazingira tunayoyakuta iwapo si mazuri, baadaye tunakaa miezi mitatu au sita na kufuatilia utekelezaji. Iwapo tutkuta wamefanya dharau tunachukua hatua zaidi," alisema mkurugenzi huyo.

Naye Afisa Zimamoto kutoka Makao Makuu, Mohammed Haji, alitaka viongozi wa hoteli hiyo kuwashirikisha zimamoto na uokozi wakati wanapotaka kujenga miundombinu ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza.

Pia alishauri kuweka chupa za kuzimia moto katika sehemu ya kufulia ili kuweka usalama kwa wafanyakazi wao na kushauri kuweka visanduku vya huduma ya kwanza pamoja na vifaa maalumu kwa Watu wa usafi ikiwemo Barakoa ili kujikinga na madhara yanayoweza kujitokeza.

Meneja wa Hoteli, Jacob Makundi, aliahidi kushirikiana na watendaji wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar na taasisi zingine ili kufuata utaratibu na kuimarisha utendaji wa kazi.

# Mapinduzi yafanikisha uhifadhi mazingira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Suleiman Said, amesema kumekuwa na mafanikiio makubwa katika hifadhi na utunzaji mazingira ndani ya miaka 60 ya Mapinduzi za Zanzibar yaliyofanyika mwaka 1965.

Ametaja miongoni mwa mafanikio hayo kuwa ni kuondoa wastani wa tani 360 za kemikali hatarishi zilizomaliza muda wa matumizi ambazo zilikuwa zimehifadhiwa katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba.

Akizungumza jana na waandishi wa habari visiwani hapa, alisema kemikali hizo zililetwa kwa ajili ya matumizi ya afya, kilimo, viwanda na matumizi ya maabara za shule na kutokana na kumalizika muda wa matumizi na kuwa hatarishi, zimekusanywa na kupelekwa Uingereza kwa ajili ya uangamizaji salama kwa mazingira na afya ya jamii.

Waziri alisema pia wizara yake imefanikiwa kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo ilikuwa tishio kwa uharibifu na uchafuzi wa mazingira pamoja na afya kwa jamii.

"Mafanikio makubwa yamepatikana katika udhibiti wa mifuko hiyo na kuifanya Zanzibar kuwa miongoni mwa nchi za kupigiwa mfano katika udhibiti wa mifuko ya plastiki. Kwa ujumla, mifuko ya plastiki imepungua kuzagaa mitaani kama ilivyokuwa imezoeleka siku za nyuma," alisema.

Pia waziri huyo alisema serikali imeendelea kuhakikisha miradi ya kiuchumi na maendeleo inayoanzishwa Zanzibar inazingatia usimamizi wa mazingira kwa kufanya tathmini za athari za kimazingira na ukaguzi wa kimazingira.

Waziri huyo alisema kuanzia mwaka 2015/16 hadi Desemba, mwaka jana, miradi 642 imefanyiwa tathmini za kimazingira na miradi 34 imefanyiwa tathmini ya athari za kimazingira mwaka 2015/16 na miradi 136 imefanyiwa mwaka 2022/23, hivyo kumekuwa na ongezeko la miradi 102.

Alisema ongezeko hilo linatokana na juhudi za serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuhakikisha miradi ya kiuchumi na kimaendeleo inazingatia masuala ya mazingira wakati wa uanzishwaji na utekelezaji.

Pia alisema vyeti vya kimazingira hutolewa kwenye miradi hiyo ambavyo huambatanishwa na masharti ya kimazingira na vyeti hivyo kwa ajili ya kuhakikisha miradi inaendeshwa bila kuwa na uharibifu na uchafuzi mkubwa wa mazingira.

"Serikali imefanikiwa kujenga mtambo wa kusafisha maji taka katika eneo la Msingini, Chake Chake kisiwani Pemba pamoja na msingi wa kupitisha maji ya mvua wenye urefu wa mita 100 katika eneo hilo," alisema.

Harous alisema kuwapo kwa mtambo huo kunasaidia kupunguza utiririshaji wa maji taka na hatimaye uchafuzi wa mazingira ya bahari ya hifadhi ya mkondo wa Pemba.

Hata hivyo, alisema katika juhudi za kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, serikali imeandaa na kuzindua mkakati wa Zanzibar wa mabadiliko ya tabianchi wa mwaka 2014 ambao unatoa dira ya hatua za serikali na wadau zinazotakiwa kuchukuliwa za kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.



Mkurugenzi Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto Zanzibar, Dk. Salum Rashid (kushoto)akiwa na wadau kutoka sekta za umma, binafsi na washirika wa maendeleo wakijadili uanzishwaji wa jukwaa la wadau ambao wanashughulikia maendeleo ya watoto Zanzibar, Kinazini Unguja juzi. P**ICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri asema ujenzi barabara umeleta maendeleo, ajira vijana

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, amesema ujenzi wa barabara ya Kombeni, Nyamanzi na Dimani na vitongoji vyake ni kichocheo cha maendeleo na upatikanaji wa ajira kwa vijana.

Aliyasema hayo jana Nyamazi Wilaya ya Magharibi B Unguja wakati wa uzinduzi wa barabara hizo kufuatia shamrashamra za maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema wananchi wa maeneo hayo kwa muda mrefu walikuwa na malalamiko ya barabara lakini kujengwa kwake kutaondosha changamoto walizokuwa wakizipata hasa wanapokuwa na watoto, wagonjwa na mizigo.

Mazrui alisema maeneo hayo yamo katika maeneo yanayokua kwa uwekezaji na ujenzi wa majengo ya kisasa jambo ambalo litaufanya mji huo kuwa wa pili kwa Zanzibar.

"Hapa zitatokea ajira na mkongo wa mawasiliano unajengwa hapa. Maonyesho ya biashara yapo hapa, majengo mazuri yapo hapa. Huu utakuwa mji wa Pili na utatoa fursa za ajira kwa vijana wengi" alisema Mazrui.


Pia alisema ujenzi huo ni kuyaenzi Mapinduzi yaliyomkomboa mnyonge kutoka katika makucha ya wakoloni sambamba na kuwaletea maendeleo endelevu wananchi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Shomari Omar Shomari, alisema barabara hiyo ina urefu wa kilomita 2.8 inajengwa kwa kiwango cha uwekaji wa tabaka lake mikali iliochanganywa na maji, uwekaji wa tabaka mbili za lami ya kokoto (chipsi) na uwekaji wa tabaka la lami na rojo.

Alisema barabara hiyo inajengwa na Kampuni ya IRIS ASER kutoka Uturuki na ujenzi ulianza Julai 17, 2022 na kukamilika Oktoba 5, mwaka jana na magari yanayotakiwa kupita ni ya tani 10 na inaaminika kudumu kwa mda wa miaka 10.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa, alisema ujenzi huo utaondoa changamoto kwa wananchi na wawekezaji na kuwa katika mazingira mazuri.

Gharama za ujenzi huo zimechanganywa kwenye jumla ya mradi wote wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 ambazo zake zinakisiwa kuwa ni zaidi ya Dola 800,000 za Marekeni.



BRITNEY UKURASA 14

JUMAMOSI JANUARI 6, 2024

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE



# AMEANZA VIZURI 2024

MWIGIZAJI wa filamu nchini, Zaylisah amesema uhusiano wake na Haji Manara, umemfungulia dunia mpya iliyojaa furaha tofauti na watu wengine wanavyoona wakiwa nje.

Akizungumza hivi karibuni, mrembo huyo ambaye alikuwa mke wa mwanamuziki wa Singeli, Dulla Makabila, amesema anachokiona kutoka kwa Manara ni upendo,kujali na kuthaminiwa kulikopitiliza.

"Manara ni mtu mzuri sana anatunza na anajali kupitiliza, kila mtu anasema kile anachokiona na mimi vitu hivi ndivyo nakutana navyo kila siku kutoka kwake," amesema Zaylisah.

Akizungumzia maendeleo ya uhusiano wao, Zaylisah amesema kwamba anamuomba Mungu awarahisishie kuingia katika ndoa kwani kinachofanyika sasa ni kinyume na dini ya Kiislam.

"Mimi ni mwanamke na yeye mwanaume tena aliyekamilika na anakula na kushiba ni lazima mtakutana kimapenzi, kweli ni dhambi lakini kwa kuwa tunaishi pamoja hatuwezi kuepuka, ninachoomba suala la ndoa likamilike ili tuhalalishe uhusiano wetu," ameongeza kusema.

Kwa upande wa mume wake wa zamani Makabila, Zaylisa amesema hana matatizo naye kwa sababu wanaishi bila uadui licha ya kuachana.



BASI SAWA

## J Zebrah afungua mwaka na 'Niwekee'

MSANII chipukizi wa Bongo Fleva, J Zebrah, amewaomba mashabiki kuendelea kumuunga mkono kwa kuipokea ngoma yake mpya, 'Niwekee' ambayo imekuwa kama zawadi ya mwaka mpya kwao.



Akizungumza na BT, Zebrah amesema wimbo huo ambao umefungua 2024, amemshirikisha rapa Rasco Sembo na tayari unapatikana kwenye mitandao yote.

"Nimefungua mwaka kitofauti na wimbo huu ambao nashukuru tayari unafanya vizuri mtandaoni. Niwekee ni ngoma flani ambayo mpenzi yeyote wa muziki lazima atafurahia kusikiliza maana utamgusa," amesema J Zebrah.

## Idea Tz amvulia kofia Baraka Da Prince

MSANII anayekuja kwa kasi katika muziki wa Bongo Fleva, Idea TZ, amempa heshima Baraka Da Prince kwa kumshirikisha kunogesha ngoma yake mpya Mkong'oto.

Akizungumza na BT jana, Idea alisema Baraka amekuwa akimsaidia kwenye safari yake ya muziki hivyo hakupata shida kumualika kwenye kolabo hiyo iliyotoka wiki hii.

"Unaweza kuona Baraka ananipa sapoti kubwa mpaka kuniposti kwenye instagram yake, nashukuru amefanya jambo kubwa sana kwenye wimbo wangu Mkong'oto ambao unafanya vizuri kwa sasa mtaani," amesema Idea.






## WIGI LA ZUCHU HATARI TUPU

WIGI la nywele bandia ambalo linadaiwa kununuliwa kwa shilingi laki saba na Msanii nyota nchini Zuchu, limeibua taharuki katika mitandao ya kijamii.

Kulingana na taarifa kutoka kwa duka ambalo msanii huyo alikwenda kununua, wigi hilo lina thamani ya dola za Kimarekani 4,500, shilingi milioni 11.3

Baadhi ya watu wameonyesha kuwa na wasiwasi kuhusu gharama halisi ya nywele hizo wakisema inawezekana imewekwa chumvi.



## Beka Flavour ungejitahidi kulipa

BAADA ya kuwa kimya mwaka ulipita, msanii wa muziki wa Bongo Fleva, Beka Flavour, ameibuka na kuwataka Watanzania kumchangia shilingi milioni 22 za mahari ili aanze 2024 akiwa na furaha.

Katika machapisho yake kwenye kurasa yake ya Instagram, Beka Flavor alisema mwaka uliopita umekuwa mbaya kwake kutokana na mpenzi wake kumkimbia baada ya kushindwa kulipa mahari.

Fleva alisema kwamba baada ya mkewe kuondoka, wazazi wake walimwekea vikwazo vingi ikiwemo sharti la kulipa mahali kama akitaka arudi kake

## NGOMA 5 ZILIZOTIKISA 2023

**Na Adam Fungamwango**

UMEINGIA mwaka mpya wa 2024 ambapo mashabiki wa muziki wa bongo fleva sasa wanataka kuona nani ataingia kwa kishindo.

Mwaka uliopita ulikuwa wa mafanikio makubwa kwa wasanii wa bongo fleva kwani walitoa ngoma nyingi kali na zilizotikisa si hapa nchini tu, bali Ukanda wa Afrika Mashariki na Afrika nzima kwa ujumla.

Kabla ya hatujaanza kuzisikia ngoma za mwaka huu, tujikumbushe baadhi ya nyimbo zilizotia fora na kutikisa mwaka jana.

Zipo nyingi, lakini hizi hapa ni zile tano zilizofanya vema na kuwachizisha mashabiki wengi wa muziki kiasi.

**1. Yatapita- Diamond Platnumz**

Ngoma hii iliachiwa mwanzoni mwa mwaka jana. Ilikuwa ni Januari 23 na ilizidi kumuongezea heshima msanii Diamond.

Mara nyingi, wasanii wa bongo fleva, akiwemo yeye mwenyewe hupenda kuimba nyimbo za mapenzi zaidi kuliko matatizo au changamoto zilizopo kwenye jamii.

Hata katika mapenzi tu huwa kuna changamoto, lakini wasanii wengi huwa hawaziimbi.

katika ngoma hii, Diamond alikuwa akimwambia mpenzi wake kuwa matatizo ya kipato waliyonayo kwa sasa ni ya muda. Tabu wanayoipata ni ya muda, yatapita, watayasahau na kwao itabadi ni historia tu.

**2. Enjoy- Jux Ft Diamond Platinumz**

Kama kuna ngoma iliyowatia wazimu mashabiki wa muziki basi ni hii. Jux, akishirikisha Diamond Platinum wakatoabonge la ngoma ambalo kama ukilisikiliza sana lilikuwa bomba sana kwa watu wenye stresi mbalimbali za maisha ya mapenzi.

Kwanza kabisa biti ya dude lenyewe ni la kuchezesha. Unaweza ukacheza hadi basi tu. Maneno yenyewe sasa.

Unaambiwa bora uinjoi tu, maisha yenyewe mafupi, hivyo usiyafanye magumu sana, uyafanye yawe rahisi, kwa nini ujitie mawazo. Ngoma hii ilifyatuliwa Agosti 7 na kuwafanya mashabiki kuwa kama vichaa.

**3. Pita Huku-Dulla Makabila**

Ulipotoka tu, ulileta mjadala mkubwa na baadaye ukasimamishwa. Wimbo huu ulio kwenye mtindo wa singeli, Dulla Makabila alitunga mashairi na kuangalia vitu nyuma ya pazia, ambapo watu baadhi ya watu wakawa hawamuelewi.

Mlevi kuingia peponi, na watu kama madaktari na mahakimu kwenda motoni ni vitu ambavyo kwa mtazamo wa kibinadamu hauaminiki.

Mtunzi aliona kwa uwezo wa Mungu inawezekana kwa sababu huwa hamuangalii mtu alivyo bali moyo wake.

Yoyote anaweza kuwa mzuri kwenye macho ya jamii, lakini nyuma ya pazia ni mtu mbaya, katili.

hayo anaweyeza kuyaona ni Mungu pekee. Baadaye walioufungia wimbo wakamuelewa, na kuufungulia. Ni wimbo uliotikisa mwaka jana, ingawa ulitoka mwishoni mwa mwaka 2022, Desemba.

**4. Amepotea-Mbosso**

Mei 11 mwaka jana, Mbosso alipotea. Akatoa ngoma ambayo ilionyesha kuwa anatafutwa na hajulikani alipo.

Watu wakatoa matangazo sehemu mbalimbali, ikiwemo vipeperushi, kumbe jamaa ameweka ndani mwanamke.

**5. -Tajiri- Lavalava**

Moja kati ya ngoma vilizokuwa zinavutia kutazama video yake ni hii iitwayo 'Tajiri.'

Maudhi yake yale yale, tajiri hanuniwi. Unaelezea tabia ya baadhi ya watu ambao kazi yao ni kukaa na matajiri wakiwasifia maarufu kama 'uchawa' ili kununuliwa pombe, nyama choma na chakula. Ngoma ilitoka Juni 30 mwaka jana.

FILAMU

## Nalipiza: Kisasi ni haki yangu

**Na Adam Fungamwango**

MKUKI kwa nguruwe, lakini kwa binadamu mchungu. Ni msemo wa kiswahili ambao maana yake ni kwamba siku zote binadamu anapokwenda kuwinda mnyama na kumuua inakuwa ni sherehe kwa familia nzima kwa sababu wamepata kitoweo

Lakini mnyama anapofanya hivyo kwa binadamu inakuwa balaa. Ni kilio na kusaga meno, watu mpaka wataandamana kwa nini mnyama ameua mtu.

Hiyo ipo hata kwa binadamu kwa binadamu. Ndipo msemo unapotimia, kuna watu wanapenda kuwafanyia ubaya wenzao, lakini wakifanyiwa wao inawauma kuliko kawaida.

Mfano tunaouna katika filamu hii ya 'Nalipiza.' Imechezwa na Ibrahim Kitimbu, Rolando Momo, Salhath Said, Warda Abbas, Latifa Mgeni, Tunu Kilindo, na wengineo.

Momo, kijana mmoja mtaani hapo, anaanzisha uhusiano na msichana Kizibo ambaye pamoja na umri mdogo lakini pia ni mwanafunzi.

Modrick, kaka yake Kizibo anajaribu kumwambia jirani yake Momo pia anavyofanya si vizuri lakini anapewa maneno ya dharau na kejeli.

Anamfuatа pia dada yake kujaribu kumuasa aachane na Momo, badala yake akili yake ielekezwe kwenye masomo lakini, akaambulia matusi, mpaka akaamua kukaa kimya na kuwaacha wafanye wanavyovitaka.

Momo naye ana dada yake. Anaitwa Esma. Modrick akaamua kulipiza kisasi. Akaanzisha uhusiano wa kimapenzi na dada wa shemeji yake.

Ngoma ikawa droo, Modrick na Esma na Momo na Kizibo. Modrick akaona kama haitoshi. Bado haimuumi. Akaanzisha uhusiano wa kimapenzi na mama yake Momo.

Momo alipogundua hilo alimsemea ovyo mama yake, lakini akakutana na onyo kali la amri ya mzazi kutoka kwa mama yake akawa kimya. Hii sasa ikaanza kumuuma Momo.

Ikawa kama haitoshi, akaanzisha uhusiano mwingine na shangazi ya Momo.

Momo mwenyewe aligundua uhusiano wa Modrick na familia yake, ambao wote hawataki kusikia suala ya kuachana na mtu huyo.

Alipokwenda kuomba ushauri kwa dada mmoja jirani alimpa ukweli kuwa mwenzake anafanya yote hayo kutokana na kisasi cha yeye kumchukua dada yake ambaye ni mwanafunzi na alipomshauri alimpakia maneno ya dharau.

Momo alipoona hivyo akaenda kuomba radhi kwa mama yake, dada na shangazi yake kuwa amewasababishia matatizo kwa kutembea na dada wa Modrick kiasi kwamba kwa sasa analipiza kisasi.

Akaenda kumuomba pia msamaha Modrick na kuahidi kuachana na dada yake.





# Yul amchamba mke wa zamani

STAA wa filamu kutoka Nollywood, Yul Edochie amemkabili kwa mara nyingine mkewe wa zamani May Yul-Edochie, kwa kumuita muongo na mdanganyifu.

Edochie amesema kwamba yeye amekuwa muungwana kwa May hadi amekubali kutumia jina lake la mwisho kama njia ya kuonyesha upendo lakini linapokuja suala la kurudishiwa mahari yake yeye na familia yake wamekuwa hawataki.

"Umeomba talaka wewe mwenyewe, lakini ulikataa kuacha kutumia jina langu. Nakuomba rudisha mahari niliyolipa, inakuwaje wewe na familia yako mnakataa sielewi kwanini," ameandika Edichie.



## Britney hataki tena muziki

MASHABIKI wa mwanamuziki wa Marekani, Britney Spears, wamekuwa na huzuni baada ya msanii huyo kutangaza kuachana na muziki.

Spears amewaambia mashabiki wake kupitia ukurasa wake wa Instagram kwamba wasisikilize uvumi wa watu kwamba anataka kutoa albamu mpya kwa sababu amefikia mwisho wa maisha ya muziki.

"Wanaendelea kusema kwa kubahatisha kwamba nimekamilisha albamu mpya, mimi sitarudi kwenye tasnia ya muziki. Nitaandika tu kwa ajili ya kujifurahisha au kwa watu wengine," amesema Spears.

## L.A.X amtisha mtumiaji wa X

RAPA mkali kutokaNigeria Damilola Afolabi, maarufu kama L.A.X, sasa anatishia kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mtumiaji wa mtandao wa X, kwa kumtusi.

Tukio hilo lilianza baada ya mpenzi wa msanii huyo kuweka ujumbe wa kumtakia heri ya mwaka mpya katika mtandao huo, ndipo watu mbalimbali walianza kutoa maoni akiwamo Edna_Reese ambaye alimwita kwa jina ambalo anaamini kama matusi kwake.

Maoni ya Reese yalionekana kupendwa na mamilioni ya watu kiasi ambacho kilimfanya msanii huyo kutoa anagalizo la kumshitaki Reese kwa kauli yake hiyo.





## Rema, Justine waibua gumzo

Hivi karibuni mitandao nchini Nigeria imezidi kuelemewa na watumiaji baada ya kuibuka tetesi ya wanamuziki maarufu Rema na Justine Skye kutoka Marekani wana uhusiano wa kimapenzi.

Uvumi huo ulianza mara video iliyowaonyesha wawili wakitoka nje ya kanisa pamoja wakiwa wamezungukwa na walinzi.

Saa chache baada ya kuonekana kwa video hiyo, watumiaji wa mitandao ya kijamii walianza kuandika maoni yao huku wakielezea hisia zao kuwa wananvyoonekana wawili wana uhusiano wa kimapenzi.

## Msaidieni Zack Orji

Zack Orji, ambaye pia ni mwigizaji ametoa maombi hayo baada ya Waziri wa Sanaa, Utamaduni kumtembelea mume wake hospitalini ambako anapatiwa matibabu.

Zack anatakiwa kufanyiwa upasuaji wa ubongo na waziri huyo akaahidi kuanzisha mchango kwa wananchi ili kupata fedha hizo.

"Mungu atamponya na atakuwa mzima. Tutafanya yote tuwezayo ili kumuunga mkono. Tunaomba maombi ya pamoja ya Wanijeria kwa sababu yeye ni kama sehemu ya familia zetu. Tumemtazama akituburudisha na tunamuona ni tunu ya taifa," amesema waziri.



# Waziri akunwa huduma usafiri

**Na Allan Isack,** LONGIDO

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, ameridhishwa na utoaji na upatikanaji wa huduma kwa wasafiri wanaopitia mpaka wa Namanga, unaozitenganisha Tanzania na Kenya.

Aliyasema hayo jana wilayani hapa wakati wa ziara yake ya siku moja ya kukagua na kuangalia hali halisi ya utendaji kazi na utoaji huduma katika mpaka huo kwa wasafiri, mali na mizigo na magari ya mizigo.

Katambi alisema serikali kwa sasa inaridhishwa na huduma zinazotolewa na maofisa wake katika Kituo cha Huduma za Pamoja Mpakani (OSBP) kilichoko wilaya ya Longido, mkoani Arusha.

"Licha ya kuwapo kwa kituo cha pamoja kuwa na mifumo inayowarahisishia abiria kupita mpakani, ni vyema kuzingatia hali ya usalama mipakani kwa kufanya kwa umakini upekuzi wa abiria, mizigo na magari ya mizigo ili kujiridhisha kuwa raia wanaovuka mpaka wanakuwa na vibali halali.

"Lakini pia kwa ajili ya kuzuia upitishaji wa bidhaa za magendo. Nimeona mifumo bora ya kuhudumia wasafiri inayodhibiti watu kupita bila vibali muhimu," alisema.

Awali, Ofisa Mfawidhi wa Uhamiaji Namanga, Mrakibu wa Uhamiaji Bulugu Mkanga, alimweleza Naibu Waziri kwamba kituo hicho kina ofisi 18 za taasisi zinazohusika na usafiri wa mpakani.

Pia alisema kuna makubaliano ya pamoja kati ya Tanzania na Kenya yanayoruhusu raia wa nchi hizo mbili kutembea hadi kilomita 20 kwa pande zote. Alisema hali hiyo imesaidia kupunguza uhalifu na kuongeza mwingiliano wa amani wa kijamii na kibiashara katika eneo la Tanzania.

"Kupitia makubaliano hayo, raia wa Kenya anaruhusiwa kuingia hadi kipenyo cha kilomita 20 katika eneo la Tanzania. Kadhalika na raia wa Tanzania anaruhusiwa kuingia Kenya kipenyo hicho hicho bila kuwa na kibali chochote zaidi ya kitambulisho cha utaifa tu jambo ambalo limefanikiwa na kuongeza muingiliano wa kibiashara mpakani.

# Kicheko wapagazi nyongeza malipo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KIMEELEWEKA. Ndivyo inavyoweza kuelezwa baada ya serikali kuwabana waendeshaji wa sekta ya utalii nchini kuongeza kiwango cha malipo ya wapagazi kwa siku kutoka Dola 10 za Marekani hadi kufikia Dola 15.

Kuanzia Januari Mosi, mwakani, wapagazi wote nchini watalipwa Dola 15 za Marekani, sawa na Sh. 35,000 za Tanzania na fedha hizo hazitakuwa taslimu badala yake zitalipwa kwa njia ya benki.

Katibu Mtendaji Chama cha Wapagazi Tanzania (TPO), Loishiye Mollel, alidokeza jana kuhusu neema hiyo wakati wa hafla ya kusherehekea makubaliano hayo baada ya kilio cha muda mrefu cha wapagazi.

"Tunaomba wadau wa utalii pamoja na serikali, kuheshimu kuyatekeleza ili wapagazi wafanye kazi kwenye mazingira bora na kuleta ufanisi kwa wageni na taifa kwa ujumla.

"Iko hivi, malipo ya Dola 10 kwa siku yataendelea hadi Desemba 31, mwaka huu, na baada ya hapo, wapagazi watapaswa kulipwa Dola 15, sawa na 35,000 kwa siku wanapopandisha mizigo ya wageni kwenda katika kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro.

Katibu Mtendaji wa Chama cha Wamiliki wa Kampuni za Utalii Tanzania (TATO), Sirili Akko, alisema katika kutekeleza makubaliano hayo, walikubaliana wapagazi wote watalipwa kwa njia ya benki baada ya kupata namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN).

Alisema njia hiyo ya kibenki itasaidia kujua baadhi ya wamiliki ambao hawawalipi Wapagazi kiwango kilichokubaliwa.

"TATO tupo tayari kutekeleza makubaliano, lakini lazima malipo yote yafanyike kwa mfumo wa kielektroniki. Tutachukua hatua dhidi ya wachache ambao hawatafanya hivyo.

"Sisi tutahakikisha maslahi ya Wapagazi yamekamilika kamatulivyokubaliana. Ila na nyinyi mtusaidie katika usafi wa mlima na usalama wa mgeni kwa wakati wote mtakapokuwa naye huko mlimani, ili mwisho wa siku wageni waongezeke zaidi," alisema Akko.

Mwakilishi wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Alexander Lemunge, alisema serikali iko tayari kusimamia makubaliano hayo, huku ikiwakumbusha wamiliki kufanya makubaliano bila kusuasua.

Aidha, Ofisa Elimu kwa Mlipakodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoani Kilimanjaro, Odupai Papaa, aliwataka wapagazi hao kutoa taarifa walipo na watafutwa na kuandikishwa ili kupata namba ya mlipakodi.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Cuthbert Sendiga, akizungumza jana na wakazi wa kijiji cha Gendabi wilayani Hanang' waliopatwa na maafa yaliyosababisha vifo, majeruhi, nyumba kubomoka, mashamba kutuama maji na mifugo kupotea. **PICHA: GIFT THADEY**

# Uandikishaji wanafunzi darasa la kwanza wadoda

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKOA wa Arusha unajikongoja katika uandikishaji wa wanafunzi wapya wa darasa la awali baada ya kuwasajili kwa asilimia 56 pekee, sawa na watoto 39,054, huku darasa la kwanza ikiandikisha wanafunzi 46,002.

Kwa mujibu wa Kaimu Ofisa Elimu wa Mkoa, Emmanuel Mahundo, walioandikishwa kuanza darasa la kwanza mwaka huu ni sawa na asilimia 74.

"Lengo la mkoa ni kuandikisha wanafunzi wa darasa la awali 69,174 na wanafunzi 62,307 wa darasa la kwanza. Lakini bado hatujafikia lengo kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za kifamilia.

"Kimsingi tunategemea kufikia lengo hili, baada ya shule kufunguliwa Januari 8, mwaka huu. Niwaombe wazazi na walezi kuwapeleka watoto shule zinapofunguliwa licha ya uandikishaji kuanza tangu Oktoba, mwaka jana," alisema.

Pia alisema serikali imetoa fedha nyingi kupitia Mradi wa Kuimarisha na Kuboresha Elimu ya Awali na Msingi (BOOST) kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya kisasa na samani zake, hivyo kila mzazi au mlezi mwenye mwanafunzi wa kuanza darasa la awali mwaka huu, ahakikishe anampeleka mtoto shule kwa kuwa elimu ni bure.

"Wazazi na walezi hakikisheni watoto wote wenye umri wa kuanza darasa la awali na darasa la kwanza, mnawapeleka shuleni kuandikishwa na hakuna gharama zozote kwa sababu serikali imetoa fedha nyingi kupitia mradi wa BOOST, ili watoto wetu wapate elimu ambayo inatolewa bure bila malipo,"alisema.

Kuhusu walimu wakuu na walimu, Mahundo aliwataka kutoweka vikwazo vya aina yoyote katika kuwapokea wanafunzi wa awali na wa madarasa mengine, ikiwamo sare na michango ambayo wazazi wameridhia.

"Si sahihi kwa waalimu wakuu na waalimu kuwarudisha watoto nyumbani kisa hana sare ya shule. Watoto waendelee na masomo wakati wazazi wakiendelea kukamilisha sare pamoja na mahitaji mengine, ikiwemo michango ambayo kamati ya shule imeridhia pamoja na wazazi," alisisitiza.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# KWELI SASA KUMEBADILIKA

## -Mwaka mpya, madebe, mabati, moto wa matairi sasa kimya

Na Adam Fungamwango

TUMEUONA mwaka mpya wa 2024 baada ya kukamilika siku 365 za 2023.

Tumeshuhudia na kusikia shamrashamra za kukaribisha mwaka mpya sehemu mbalimbali nchini, maeneo kadhaa tu nchini na kwenye mahoteli makubwa.

Niseme tu kwa miaka ya karibuni sherehe hizo hazivutii mitaani kama miaka ya zamani.

Tulichoshuhudia ni kuona baadhi ya watu tu kwenye maeneo machache wakirusha miale ambayo inatawanyika juu na kufanya kama ua hivi.

Mitaani tumeshuhudia tu makundi ya vijana wakijikusanya, wengine wakinunua vinywaji na kukaa vikundi vikundi wakionekana kama kujadiliana tu vitu fulani kama vile vikao vya familia linapotokea tatizo.

Wengine hasa watu wazima wakienda baa za jirani wao wenyewe au mtu na mkewe kupata moja moto, moja baridi.

Kwa tathmini yangu sherehe za kuukaribisha kwa miaka ya hivi karibu mitaani ni kama zimedoda kabisa.

Watu hawana lile 'vaibu' kama la zamani ambalo sisi watu wa miaka ya nyuma kidogo tumepata kushuhudia.

Kwa sasa watu hawasherehekei vile ambavyo sisi wengine tunafahamu huko nyuma dakika 10 kabla ya kuingia mwaka mpya na saa nzima baada ya kuingia 'mtiti' wake ulikuwaje.

Inawezekana kizazi cha sasa hawajui jinsi gani ya kusherehekea mwaka mpya kwa sababu hata watoto tu wanajikusanya majumbani mwao kimya, wakiusubiri, na hata kama ukiingia kila mmoja anakuwa kwenye televisheni akiangalia unaingiaje.

Wanachoshindwa kufahamu kuwa hata humo kwenye televisheni kunatakiwa kuwe na watu waliochamgamka ili na wao waone raha kutazama shamrashamra za mwaka mpya.

Wataona wapo wakati kila mmoja amekaa nyumbani kwake kimya?

### 'VIBE' LA MWAKA MPYA HUKO NYUMA

Niwajuze tu vijana wa sasa kuwa miaka ya nyuma sana, hadi kabla ya miaka minne nyuma, dakika 15 kabla mwaka mpya kuanza hata kama umejifungia peke yako chumbani, utapata habari kuwa mwaka mpya unawadia.

Kelele za honi za magari zisizo za kawaida zinakushtua na kumuambia kuwa nje huko kuna mambo.

Halafu itafuatia milio mikali ya fataki, ikiashiria kuwa mwaka wa zamani unaondoka na mpya unaingia.

Ile inapotimia saa sita kamili sasa unaweza ukadhani kuna mvua kubwa inanyesha. Kelele za watu, wakubwa na wadogo wakiashiria wameingia kwenye jahazi lingine la mwaka mpya.

Sasa kuna wale ambao wanakusanyana kama vile timu ya mpira imeshinda. Wanaanza kitu fulani hivi, mchakamchaka si mchakamchaka, maandamano si maandamano, wanapita mitaani wakiwa wanaimba na kucheza.

Hawa wanakuwa na madebe, na makopo ambayo yanapigwa kwa nguvu zote katika kusherehesha kuingia kwa mwaka mpya.

Hapo hakuna mtu ambaye anakuwa amelala, si mkubwa si mtoto, kile mtu yuko macho na siyo ndani, nje.

Kama atakuwa anaangalia wale ambao wanacheza na kupita na vigoma na madebe sawa, au na yeye atakuwa mmoja wa watu waliolisakata sebene la vigoma, madebe, mabati na makopo na kukatisha mitaa.

Kuna wale ambao walikuwa wanavuka mipaka na kwenda mabarabarani au njiani na kuchoma moto matairi.

Aina hii ya ushangiliaji hukatazwa na Jeshi la Polisi na wanaofanya hivi hutiwa mbaroni, ndiyo maana hadi leo, siku chache kabla ya mwaka mpya hutoa tahadhari na kuonya wale wote wanaotaka kuchoma matairi.

Kwa sasa hii haipo kabisa, kwanza hata hayo matairi mabovu yenyewe kwa sasa ni adimu sana, sijui watayapata wapi ya kuyachoma.

Kwa sababu huo ni wajibu wao tu Jeshi la Polisi, lakini kwa sasa hata kama wasipotoa tahadhari, kama wapiga makopo na madebe tu sasa hivi hakuna, sidhani kama kuna kuchoma matairi.

Tukirudi sasa kwenye sherehe zizokuwa zilizoruhusiwa na Jeshi la Polisi, sherehe za madebe, ngoma zinafanyika karibuni saa nzima mitaani baada ya kuingia mwaka mpya, kabla ya kurudi kwenye hali ya kawaida.

Pilikapilika zingine zitahamia kwenye kumbi za burudani na starehe, kabla ya maisha mengine kuendelea kunapokucha.

### SASA UPO KAMA HAUPO

Tukija miaka ya hivi karibuni ni kama vile upo kama haupo. Inaonekana kama vile kizazi cha sasa wanachukulia poa hivi.

Au inawezekana uzungu mwingi umewaingia, kwani hatuoni lile 'vibe' la miaka ya nyuma kama nilivyoainisha hapo mwanzo.

Utaona yale mafataki ya miale tu yanayochanua kama maua, lakini zile fataki zenye mshindo kaama baruti, au baruti zenyewe ni chache sana.

Hakuna mabati, madebe, wala makopo yanayopigwa, wala maandamano yale ya kupita mitaani kusherehekea hakuna tena.



Picha hii inaonyesha jinsi mwaka mpya unavyosherehekewa miaka ya hivi karibuni, kibosibosi

Kila mmoja anakusanya familia yake na kukaa nyumbani. Kuna vitu vichache sana vimebaki ndivyo vinaweza kukuambia kuwa haya ni majira ya saa sita usiku, mwaka mpya unaingia.

Labda tunaweza kuanza kujiuliza sababu ni nini? Awali nilivyoweka mada hii kwenye mtandao ili kukusanya maoni, baadhi walisema ugumu wa maisha umechangia kuwepo kwa hali hii na hasa unapoingia mwaka mpya, badala ya watu kusherehea wanawaza sare za shule za watoto wao, ada, kodi, gesi inakaribia kumalizika, pesa ya takataka, ya ulinzi, madeni, vyote hivi vinasababisha badala ya watu siku hizi badala ya kusherehekea mwaka mpya, wanaununia.

"Maisha yamebadilika sana mkuu, unaambiwa hata yale madebe, makopo na mabati ya kupiga yaliyokuwapo zamani siku hizi ni dili yanauzwa kama 'skrepa' ili watu waweze kujikimu," anaandika mchangiaji mmoja.

"Ila ni kweli sikusikia madebe, makopo wala mabati, hakuna fataki, kama yalikuwepo basi ni sehemu chache sana tofauti na zamani kila sehemu utasikia vishindo," anaandika mwingine.

Mwingine anasema aina ya maisha ambayo wamejiamulia kuishi kizazi cha sasa ndicho kinasababisha hayo.

"Mimi naona tu majira yamebadilika na watu wameamua kuchukulia ni jambo la kawaida na kuna kitu kama uzungu hivi, 'kuna ubrazameni, na usista duu mwingi', kiasi kwamba huwezi tena kuona watu wanazunguka na makopo mitaani."

TUMA MESEJI 0716 350534




Taswira inayoonyesha watu wa miaka ya nyuma walivyokuwa wanashangilia mwaka mpya unapoingia.

# Maandalizi utawala mpya Gaza waanza

**Gaza City,** GAZA

WAZIRI wa Ulinzi wa Israel, Yoav Gallant, ametangaza mapendekezo ya utawala wa Ukanda wa Gaza, baada ya kumalizika kwa vita kati jeshi la nchi yake na kundi la Hamas.

Miongoni mwa mipango inayowekwa na Israel, ni kuhakikisha kuwa, Gaza inaongozwa kwa kiwango kidogo na Wapalestina.

Kuhusu usalama, ukanda wote wa Gaza utakuwa chini ya Jeshi la Israel na kundi la Hamas halitaruhusiwa kuwapo.

Mapendekezo hayo, yanakuja wakati jeshi la Israel likiendeleza mashambulizi ambayo kwa saa 24 zilizopita, mauaji ya watu yameendelea kushuhudiwa.

Wizara ya Afya kwenye ukanda huo, inasema watu 125 wameuawa kwa kipindi cha saa 24 zilizopita na jeshi la Israel likiapa kuendelea na operesheni dhidi ya kundi la Hamas katika vita ambavyo vimesababisha vifo vya zaidi ya watu 22,000.

# Blinken ziarani

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, anaelekea Mashariki ya Kati, huku kukiwa na juhudi kubwa za kidiplomasia ili kufanikisha ufikishaji wa misaada ya kibinadamu Ukanda wa Gaza.

Shinikizo la kimataifa kwa Israel ni kupunguza vifo vya raia wa Palestina.

Hii ni ziara ya nne ya Blinken, Mashariki ya Kati, tangu shambulizi la Oktoba 7, mwaka jana la Hamas dhidi ya Israel.

Hamas inachukuliwa kama taasisi ya kigaidi na Marekani, Uingereza, Umoja wa Ulaya (EU) na mataifa mengine.

"Waziri huyo atatembelea Uturuki, Ugiriki, Jordan, Qatar, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Saudi Arabia, Israel, Ukingo wa Magharibi, na Misri, akiwa na mikutano na mawaziri wenzake wa mambo ya nje na wengine," Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje, Matthew Miller, alisema.

## BAADA YA KIFUNGO MIAKA 11

# Mwanariadha Oscar Pistorius aachiwa huru

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI



Oscar Pistorius. **PICHA: BBC**

OSCAR Pistorius, mwanariadha maarufu duniani mwenye ulemavu wa miguu raia wa Afrika Kusini, aliyeteka vichwa vya habari katika vyombo vya habari duniani, miaka ya 2000 ameachiwa huru.

Pistorius (pichani), ameachiwa huru kwa msamaha, jana, nchini humo, baada ya kukaa kifungoni kwa takribani muongo mmoja.

Pistorius, alihukumiwa kwa mara ya kwanza mwaka 2014 baada ya kukutwa na hatia ya kumuua mpenzi wake kwa risasi, Reeva Steenkamp, siku ya wapendanao duniani, Valentine's Day' mwaka 2013.

Tovuti ya chombo cha habari cha SABC News, kilichopo Afrika Kusini, kinaeleza kwamba bingwa huyo aliyeweka rekodi na kutwaa medali za dhahabu kwa 'kukata upepo' kwenye mbio fupi kwa wenye ulemavu, yuko huru.

Mwaka 2014, Pistorius alihukumiwa na Mahakama Kuu nchini Afrika Kusini, kifungo cha miaka mitano jela, kwa kosa la kuua bila kukusudia.

Mwaka uliofuata baada ya hukumu hiyo, Mahakama Kuu ya Rufani, nchini humo, ilimkuta na hatia nyingine ya mauaji na kupewa nyongeza ya miaka sita.

Kadhalika mwaka 2017, Mahakama Kuu iliongeza miaka ya kutumikia jela kwa zaidi ya mara mbili na kufikia miaka 13 na miezi mitano, ikisema kuwa muhula wa miaka sita, ulikuwa mdogo sana kwa kesi yake.

**PISTORIUS NI NANI?**

Maisha ya Pistorius, ambaye hadi anatoka kifungoni, akiwa na miaka 37, alikuwa maarufu kuanzia miaka ya 2000 baada ya kuondoa dhana katika jamii kwamba mtu mwenye ulemavu, hawezi kushiriki baadhi ya shughuli, ili kujipatia kipato.

Katika mashindano ya dunia ya Olimpiki mwaka 2012 huko, London nchini Uingereza, Pistorius alikuwa mwanariadha wa kwanza mwenye ulemavu, asiye na miguu kuanzia eneo la magoti kwenda chini, kuvaa miguu ya bandia kushiriki mbio fupi.

Lakini maisha yake, Februari 14, mwaka 2013, yalibadili mtazamo wake na umaarufu wake, akiangukia mkono wa sheria, baada kumuua kwa kutumia bastola mpenziwe, nyumbani kwake, Pretoria, akidhani amevamiwa na jambazi.

Alijipatia umaarufu na kupewa majina kadhaa kama 'Blade Runner', mshindi wa medali nyingi za dhahabu za Paralympic, akiwa na miguu bandia ya kaboni-fiber na mtu wa kwanza kushindana katika Olimpiki aliposhiriki katika michezo ya London mwaka 2012

Baada ya kifungo, Pistorius, umaarufu wake akikutwa na hatia ya mauaji, ikimpasa kukaa kando kwa muongo mmoja, akiwa gerezani.

Alipatikana na hatia ya kumuua mpenzi wake Reeva Steenkamp, akiwa na umri wa miaka 29, binti mwanamitindo na mhitimu wa Shahada ya Sheria, akimpiga risasi kupitia mlango wa bafuni nyumbani kwake, huko Pretoria.

Hatua ya kutoka kifungoni kwa Pistorius, ni kutokana na utaratibu wa PAROLE. Atakuwa chini ya uangalizi. Amekaa karibu miaka 11 baada ya mauaji hayo. Alipewa PAROLE, Novemba 24, mwaka Jana, na utekelezaji wake ulianza jana.

Pistorius, ambaye alizaliwa bila miguu yote miwili, ilikatwa chini ya magoti na kuwekewa ya bandia, kabla ya kusheherekea siku yake ya kuzaliwa, na kuonekana kama mfano wa ushindi wa binadamu dhidi ya shida.

Mwanariadha huyo, mzaliwa wa Johannesburg, alijipatia umaarufu duniani mwanzoni mwa miaka ya 2000, aliposhinda medali ya dhahabu ya Paralimpiki katika mbio za mita 200 kwenye Michezo ya Athens.

Kisha Pistorius alijielekeza katika kukimbia dhidi ya wanariadha wenye uwezo duniani kwenye Michezo ya Olimpiki ya Beijing ya 2008, ingawa alizuiwa kushiriki mashindano hayo na Riadha za Dunia, ikidaiwa yuko tofauti na wengine. Mbio hizo awali ziliitwa Shirikisho la Kimataifa la Riadha.

Uamuzi huo, ulibatilishwa na Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo, akasnza kushiriki michezo hiyo, ingawa Pistorius alishindwa kufuzu Michezo ya Olimpiki, baada ya sekunde 0.70 kutoka kiwango cha kufuzu cha mita 400 huko Beijing.

Hakukata tamaa, alishiriki Michezo ya Olimpiki ya Walemavu ya mwaka huo huo, akatwaa medali za dhahabu tatu katika mita 100, 200 na 400, kabla ya kufuzu kwenye Olimpiki mwaka 2012 huko London.

Katika michezo hiyo, alifanikiwa kufika nusu fainali ya mita 400 na kuwania Afrika Kusini katika mbio za kupokezana vijiti za mita 4x400.

Pia, Pistorius (37), alishinda medali nyingine tatu za Olimpiki mwaka huo huo.

Katika kesi dhidi ya mauaji ya mpenziwe, alijitetea kwamba, akiwa na bunduki, alidhani Steenkamp alikuwa mvamizi na alimpiga risasi mara kadhaa.

Awali alifungwa jela miaka mitano mwaka wa 2014 kwa kuua bila kukusudia na Mahakama Kuu. Lakini Mahakama ya Juu ya Rufani, mwishoni mwa 2015 ilimpata na hatia ya shtaka kubwa zaidi la mauaji baada ya rufani ya waendesha mashtaka.

Mwaka juzi 2022, Pistorius alikutana na baba mkwe wake, Steenkamp Barry wakati wa mchakato unaojulikana kama mazungumzo kati ya wakosaji na walalamikaji, ikiwa ni sehemu ya mpango wa urejeshani haki Afrika Kusini, ambao huleta pamoja pande zilizoathiriwa na uhalifu.

Baada ya wawili hao kukutana, maelezo machache yaliwekwa wazi kuhusu mkutano huo. Baba mkwe wake huyo, Steenkamp, alifariki mwaka jana.

Mama mkwke wa Pistorius, June, katika taarifa yake kabla ya kusikilizwa kwa PAROLE ya mwanariadha huyo, alisema kwamba hakuwa na hakika kama hukumu imerekebishwa.

Akasema alikwishasamehe kilichotokea kwa binti yake "Muda mrefu umepita nilijua hakika kwamba nisingeweza kuishi ikiwa ningeshikilia hasira yangu".

**SABC NEWS**

# HABARI PICHANI



Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo (wapili kulia) akigawa chakula kwa baadhi ya wananchi wa Manispaa ya Moshi katika kituo kikuu cha mabasi mjini Moshi mapema wiki hii ikiwa ni sehemu ya kusheherekea kuumaliza salama mwaka 2023, na kuukaribisha mwaka mpya 2024. **PICHA:JAMES LANKA**



Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu akifungua mafunzo kwa wabunge na kutoa mada inayohusu “Tathimini ya utendaji wa taasisi na ufanisi wa usimamizi wa taasisi za umma”. **PICHA:JAMES LANKA**



Wakazi wa Mabibo Kisiwani jijini Dar es Salaam, wakipita kwa shida kutokana na kivuko cha juu kuondolewa na maji, kipindi cha mvua kubwa wanalazimika kuzunguka relini. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde jana akifungua kikao cha wizara hiyo na watoa huduma kwa wamiliki wa leseni za madini nchini kilichofanyika jijini Mwanza kikilenga kusikiliza na kubaini njia za kuinua sekta hiyo. **PICHA:VITUS AUDAX**



Mfanyabiashara, Mohamed Hussen ( kulia), akipanga nazi katika soko la Temeke Stereo jijini Dar es Salaam jana. Bei ya bidhaa hiyo ni Sh. 700 hadi Sh. 400. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Wafanyakazi wa Jiji la Dodoma wakifanya usafi wa mazingira kwenye eneo linalohifadhiwa takataka lililopo soko la sabasaba jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# HADITHI

# MAMA MWENYE NYUMBA - 9

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu. Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa. Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba. Cheo hicho cha Umama wa Nyumba asiyojenga, ndiyo akawa amepata fimbo ya kuwapigia watu. Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa kama wakiishi bure au kwa mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo na mwisho wa visa vya mama huyu.

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Kwake Mwantumu ilikuwa na faida mbili. Kwanza alijua kupata kwa binti yake ni sawa na kupata kwake.

Alijua pesa atakazokuwa anapewa, chipsi, kuku, mayai, samaki, na yeye ataambulia, binti yake atabadilika, kwani anamfahamu mpangaji wake huyo Dani kuwa ni mwanaume anayejua kutunza.

Pili ni kumkomoa Devota, kwani ni mmoja wa wapangaji wake waliokuwa na adabu na heshima kwake, na kwa kuwa wamekuwa wanagombana mara kwa mara, moja katika njia za kumkomoa ni kumfanya binti yake atembee na mumewe.

Hivyo vyote vilimfanya hata asifikirie kama ikijulikana nini kitafuatia.

"Mmmh, basi nitaangalia, siwezi kusema nimekubali au nimekataa. Nipe muda."

"We mtoto wewe, hao kina Juma wanakupa nini? Ninachoona chai, vitafunio tunanyang'anyana hapa hapa na mama yako. Tafuta mtu atakayeweza kukuondolea hata shida ya kununua pesa za vitafunio mwanangu, we kalagabaho mzaramo kalonga."

"Mama nimekwambia tatizo kubwa huyu ana mke na yupo humu humu ndani mwetu. Ndiyo maana nimekwambia nipe muda. Ingekuwa hana sawa."

"Sawa nimekusikia mwanangu, ila unawajua wanaume wewe! Akizunguka huko akipata kijanamke huko kikamchezeshea macho kama kinyonga, keshakusahau. Kwa hiyo isichukue muda mrefu," Mwantumu akamtahadharisha binti yake.

Wakati Devota akidhani mkutano ule ni wa wao wenyewe, kumbe hajui anatengenezwa mbaya wake mwingine kabisa tofauti na anavyofikiria.

************************************

"Hivi Rozi, huyu mama mwenye nyumba wako anajiamini nini. Mtu alivyokondeana vile, ningemuua mimi juzi." Tabia aliongea huku akikikaa vizuri kwenye kiti, kitana mkononi akimsuka Rozi.




**"Mmmh! Mwenzangu mbona kama yanataka kuniingia maneno yako?"**

"Hapa inatakiwa hivi, kabla hatujahama tumtandike tumtupia kwenye mtaro wa maji machafu ndiyo tuhame. Na wewe Tabia ulimkunakuna tu, angeingia kwenye anga zangu yule saa hizi yupo Moi huko Muhimbili na mimi Segerea." Rozi akajibu akiwa amekaa kwenye mkeka na yeye ndiyo msukwaji.

"Ee eee, dada sasa usijitingishetingishe, nitakutoboa na kitana, ongea taratibu bila kujitikisa." tabia akamtahadharisha mwenzake.

"Si wewe ndiyo umeanza hayo mastori yako na mama mwenye nyumba wako, yaani mimi nilishasikia stori zake, mwili unasisimka, simpendi, unajua simpendi..."

"Haya basi Rozi kaa vizuri sasa nikusuke, ongea hivyo hivyo huku umekakamaa. Halafu nywele zako zina mba hizi."

"We acha tu mwenzangu, kwanza ukinisuka hapa baada ya siku tatu nazifumua nakwenda kuzikata saluni, nimechoka, mwanamke sina mafuta mimi, sina rosheni, nipo nipo tu."

"Rozi, kwa nini usimwambie bwana 'ako akununulie?"

"Tabia, siku hizi kuna wanaume basi, wanaume wenyewe nao wanaomba. Eti mara kakupigia simu na yeye anaomba eti umkopeshe kiasi fulani."

"Lo! Mwanaume wa aina hiyo mimi hata simtaki. Anipishe huko. Mwanaume amhudumie mwanamke, akatafute huko aniletee, siyo tena hata changu mimi nacho anakitaka."

"Shoga yangu tabia wapo kumi kwa mmoja, wanaume wa zamani ndiyo walikuwa hivyo, kila kitu atahudumia kwenyewe. Mwenzangu walikuwa wanajua majukumu yao, lakini wa sasa nao kama watoto tu. Mtu hajui mpenzi wake anataka kula, nguo, rosheni, mafuta, mpaka upige kelele." Akalalamika Rozi.

"Tafuta mwanaume mtu mzima Rozi, achana na hivi vivulana vitakufubaza, utakauka kama kipande cha muhogo, vyenyewe vinataka mteremko tu, kumhudumia mwanamke hawawezi, halafu na wivu juu hapo hapo."

"Mmmh! Mwenzangu mbona kama yanataka kuniingia maneno yako?"

"Oooh! We haya tu."

"Enhee tuyaache hayo Tabia, wewe mwenzangu umeshaanza kutafuta chumba?"

"Mmh! Bado, ila najua nitakipata tu"

"Shauri yako, utabaki na mama mwenye nyumba wako mwenye miguu kama miti ya kupigia ngoma ya mdundiko. Mimi nimeshaanza, ndiyo maana unaona nimekosa hata pesa ya kununulia losheni. Unafikiri mimi nategemea sana hawa wanaume wa kisasa hawa! Ila pesa yote nimeiwekeza kuhama."

"Unahamia wapi Rozi mwenzangu naona umeshapata chumba."

"Wala siyo mbali bibi wewe, na nimefanya makusudi. Sitaki nikae mbali na mama mwenye wako, nikihama ndiyo ataipata haswa. Hapa si nina mashosti zangu nyumba ya pili, nitakuwa nakuja hapa hapa."

"He! Mwenzangu kumbe wewe Rozi mtata, haya na mimi hupo jirani hakuna chumba?"

"Bado sijajua, nitakuangalizia."

"Devota je?" Tabia akauliza.

"Mwache akae waendelee kumchukulia mumewe."

"Hivi ni kweli mume wa Devota anatembea na mama mwenye nyumba?" Akauliza tena Tabia.

"Mwenangu we, si tumesikia wote pale kwenye kikao, na kasema mwenyewe Devota."

"Kaka yule naye hata simuelewi. Nini kimempeleka pale? Mwanamke kanyata, mwembamba kama kalamu, hivi unamshika wapi yule mifupa mitupu. Kha! Wanaume nao."

Wakati wakiendelea kusukana na kupiga stori za umbea, Mwantumu alikuwa anarejea kwenye mizunguko yake. Aliwaona wapangaji wake wawili wakisukana, wakipiga mastori.

Akili yake kwa haraka haraka ilimtuma kuwa walikuwa wanamteta. Hakukosea. Alinyata taratibu akiambaambaa na ukuta wa nyumba.

Kabla ya kukata kona ambapo ndipo walipokuwa wamekaa upenuni mwa nyumba yake, sikio lake liliwasikia vizuri.

Maneno waliyokuwa wanaongea juu yake walimfanya kufura kwa hasira.

Alivumilia ili aendelee kuwasikia, lakini baadaye subira ikatoweka. Akajitokeza ghafla.

"Yaani nyingi wanawake wazima badala ya kufagia vyumba vyenu vilivyojaa vilivyojaa chawa, kunguni, viroboto na mende kazi mmekalia ubea hapa, halafu mnajifanya mnasukana."

Kujitokeza kwake ghafla na kusema aliyoyasema waliwafanya Tabia na Rozi kupatwa na mshtuko.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# AZIZ KI HASHIKIKI KWA 'FRI-KIKI' LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, Stephane Aziz Ki, ameendelea kukusanya rekodi mbalimbali katika ligi hiyo, sasa akiwa ndiye kinara wa kupachika mabao kwa mipira ya faulo.

Kwa mujibu wa takwimu zetu za zile zilizotolewa na Bodi ya Ligi Kuu Nchini (TPLB)jana, Aziz Ki amefunga mabao matatu kwa mipira ya faulo hadi kufikia raundi ya 14 ya ligi hiyo, huku kukiwa hakuna mchezaji yoyote ukiondoa yeye aliyefunga mabao hata mawili kwa njia hiyo.

Takwimu za Nipashe zinaonyesha Aziz Ki alifanya hivyo katika mechi dhidi ya JKT Tanzania, Yanga ikishinda mabao 5-0, dhidi ya Azam FC, akiiongoza timu yake kupata ushindi wa magoli 3-2 na dhidi ya Tabora United, Yanga ikivuna pointi tatu kwa ushindi wa goli 1-0.


Mchezaji huyo aliyesajiliwa msimu uliopita akitokea Asec Mimosas ya Ivory Coast ameendelea kujiwekea rekodi nyingi nzuri mpaka sasa, akiwa ndiye kinara anayeongoza kwa upachikaji wa mabao mpaka sasa, akiwa na magoli 10, akiwa pia mmoja wa wachezaji wanaoongoza kwa usaidizi wa mabao.

**Nyota huyo ameisaidia timu yake kupatikana kwa mabao 12 kutokana na 'assist' zake mbili na kwenye rekodi hiyo yupo sawa na Feisal Salum 'Fei Toto' wa Azam FC.**

Kiungo huyo mwenye mashuti makali pia ndiye mchezaji anayeongoza kwa kufunga mabao mengi kwa mguu wa kushoto mpaka sasa, akiwa amepachika mabao nane.

Takwimu zinaonyesha baada ya Aziz Ki, wachezaji waliobaki wote wamefunga faulo moja kila mmoja.

Wachezaji hao ni Cheikh Sidibe wa Azam FC, Disan Galiwango (Kagera Sugar), Martin Kigi (JKT Tanzania), Ibrahim Ajibu (Coastal Union), Velentino Mashaka (Geita Gold FC), Omari Kindamba (Mashujaa FC), Marouf Tchakei na Gadiel Michael (Singida Fountain Gate) na Edwin Balua wa Tanzania Prisons.




# Ashinda 5m/- Magifti Dabodabo

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Dar es Salaam, Kiungi Nombo, ameibuka mshindi wa Sh. milioni tano katika droo ya kwanza kwa mwaka huu ya shindano la Magifti Dabodabo linaloendeshwa na Kampuni ya Tigo, imefahamika.

Nombo alikabidhiwa fedha hizo jana kwenye ofisi za kampuni hiyo jijini Dar es Salaam. Mbali na Nombo, pia mkazi mwingine wa Dar es Salaam, Christina Mrua, aliibuka mshindi wa vifaa vya umeme vya majumbani vikijumuisha, televisheni, jokofu na redio ya kisasa.

"Kwa kweli nashukuru sana kwa zawadi hii, pesa hii imekuja kipindi muhimu cha uhitaji wa pesa, nashukuru Kampuni ya Tigo kwa hiki wanachokifanya," alisema Nombo.

Mshindi huyo amewataka wateja wa kampuni hiyo kufanya miamala mbalimbali kwa kutumia Tigopesa ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kushinda kama yeye.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Huduma na Bidhaa wa Tigo, Ndevonael Eliakimu, alisema shindano hilo bado linaendelea na kuwashauri wateja kufanya miamala ya mara kwa mara ili kushinda.

Alisema zawadi mbalimbali zitaendela kutolewa na zawadi kubwa zaidi ya magari mapya itatolewa kwa mshindi pamoja na yule atakayemchagua kushinda naye.

## KenGold FC wababe Ligi ya Championship

**Na Adam Fungamwango**

MZUNGUKO wa kwanza wa Ligi ya Championship imemalizika juzi huku KenGold ikimaliza kileleni baada ya kujikusanyia pointi 35, na mchezaji wake, Edger William, akiongoza kwenye orodha ya wafungaji wa ligi hiyo, amepachika mabao 13.

KenGold, yenye maskani yake jijini Mbeya imemaliza mzunguko wa kwanza wenye mechi 15 ikipata ushindi katika michezo 11, sare mbili, ikipoteza mbili, ikifunga mabao 28, ikiruhusu tisa.

Timu nyingine kutoka Mbeya, Mbeya Kwanza inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi 32, Pamba FC ya Mwanza ikifuatia ikiwa na pointi 31, Biashara United ikimaliza mzunguko wa kwanza ikiwa nafasi ya nne na pointi 30 mkononi wakati TMA inakamilisha Tano Bora ikiwa na pointi 30 pia.

Naye Boban Bogere wa Biashara United anashika nafasi ya pili katika ufungaji akiwa na mabao 11 huku Salim Aiyee wa Mbuni FC anayewindwa wa Coastal Union kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo na Ramadhani Kapera wa Mbeya Kwanza wakiwa na mabao tisa kila mmoja.

Mchezaji wa Copco, Abdulkarim Segeja na Kassim Shaibu na KenGold, wana mabao nane kila mmoja huku Helbert Lukindo wa Biashara United na Maulid Shaaban wa Mbeya City, wakifunga mabao sita kila mmoja.

## Dodoma Jiji FC kubadili mfumo

**Na Saada Akida**

ILI kuhakikisha inafanya vyema katika mzunguko wa lala salama, Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Francis Baraza, amesema atabadilisha mfumo wa uchezaji wa kikosi chake na anatarajia kutumia mifumo zaidi ya mitatu ili kufikia malengo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Baraza, alisema kwa muda mfupi ambao amekaa na timu hiyo na namna walivyocheza katika mechi ya kwanza aliyoiongoza amebaini ndani ya kikosi kuna wachezaji wengi ambao hawakupata nafasi ya kuonyesha uwezo wao.

Baraza alisema baada ya kufanya mazoezi katika muda huu ambao ligi imesimama, atawapa nafasi nyota hao huku wengine akipanga kuwatoa kwa mkopo katika timu nyingine na kubakia na wachezaji watakaokuwa kwenye mipango yake.

"Tumekubaliana kupeleka mapendekezo hayo kwa viongozi ili kufanyia kazi kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo. Ninahitaji kuongeza watu katika safu ya ulinzi, kiungo na mshambuliaji," alisema Baraza.

Aliongeza timu yake haiko katika nafasi mbaya kwenye msimamo wa ligi na endapo watakiongezea nguvu kikosi, watapanda juu na kumaliza msimu kwa mafanikio.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### FIRMINO KUREJEA ENGLAND

FULHAM ni moja ya klabu za Ligi Kuu England ambazo zimepewa fursa ya kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Liverpool, Roberto Firmino, mwenye umri wa miaka 32, ambaye anataka kuondoka Al-Ahli ya Saudi Arabia. (***Talksport***)

### ONANA ANUKIA ARSENAL

KLABU ya Arsenal imewasiliana na kiungo wa Everton na Ubelgiji, Amadou Onana, mwenye umri wa miaka 22. Pia washikabunduki hao wanajiandaa kumsajili mlinzi wa Uholanzi, Jorrel Hato (17), kutoka Ajax. (***Telegraph***)

### SANCHO KUREJEA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund itahitajika kutoa pauni milioni 25 ili kumnunua nyota wa England, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 23 kutoka Manchester United. (***Football Insider***)

### SCALVINI KUIKAMUA UNITED

KLABU ya Atalanta inahitaji pauni milioni 51.7 kwa beki wao raia wa Italia, Giorgio Scalvini, mwenye umri wa miaka 20 ambaye anahusishwa kwenda Manchester United. (***Metro***)

### GALLAGHER KUBAKIA CHELSEA

KIUNGO wa kati wa Chelsea na England, Conor Gallagher, mwenye umri wa miaka 23, anataka kubakia Stamford Bridge licha ya kuhusishwa na mpango wa kuondoka katika klabu hiyo. (***Mirror***)

### SILVA KUREJEA FLUMINENSE

MLINZI wa Chelsea ambaye ni raia wa Brazil, Thiago Silva, mwenye umri wa miaka 39, atapewa nafasi ya kurejea katika klabu yake ya zamani ya Fluminense wakati wa majira ya joto. (***Mirror***)

### EDWARDS KUTUA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inashughulikia mpango wa kumnunua beki wa Peterborough, Ronnie Edwards, mwenye umri wa miaka 20. (***Evening Standard***)

### ZAMBRANO SOKONI EPL

BOURNEMOUTH inatazamiwa kuwasilisha ombi la kumnunua kiungo wa Timu ya Taifa ya Ecuador, Oscar Zambrano, mwenye umri wa miaka 19 kutoka Quito. (***Fabrizio Romano***)

### FRIMPONG MAMBO MAGUMU

MLINZI wa pembeni wa Bayer Leverkusen, Mholanzi, Jeremie Frimpong, mwenye umri wa miaka 23 anahusishwa na uhamisho, lakini klabu hiyo ya Ujerumani haina nia ya kumuuza. (***Fabrizio Romano***)

### AZAZ KUONDOKA VILLA

KLABU ya Middlesbrough inakaribia kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Jamhuri ya Ireland, Finn Azaz, mwenye umri wa miaka 23 kwa pauni milioni mbili kutoka Aston Villa baada ya kiungo huyo kucheza kwa mkopo Plymouth Argyle. (***Sky Sports***)

### BAILEY KUVUNJA REKODI

ASTON Villa inatarajiwa kuanza mazungumzo na winga wa Jamaica, Leon Bailey, mwenye umri wa miaka 26, ambaye anaweza kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi katika klabu hiyo. (***Mail***)

### PSG YAMFUATA EARPS

KLABU ya Paris St-Germain iko mstari wa mbele kutaka kumsajili kipa wa England na Manchester United, Mary Earps, mwenye umri wa miaka 30. (***Evening Standard***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# PISTORIUS AACHIWA HURU KWA MSAMAHA

**PRETORIA,** Afrika Kusini

**Ni baada ya kukaa gerezani miaka 11 akitumikia kosa la...**

MWANARIADHA wa zamani wa Olimpiki mwenye ulemavu wa miguu, Oscar Pistorius, ameachiwa huru jana kwa msamaha nchini Afrika Kusini baada ya kukaa gerezani kwa takribani miaka 11 kwa kosa la kumuua mpenzi wake, Reeva Steenkamp.

Alimpiga mpenzi wake risasi kadhaa kupitia mlango wa bafuni mwaka 2013 na kudai alidhani ni mwizi.

**Pistorius, ambaye sasa ana umri wa miaka 37, alipatikana na hatia ya mauaji mwaka 2015 baada ya Mahakama ya Rufaa kubatilisha hukumu ya awali ya mauaji bila kukusudia.**

Hata akiachiwa huru, bado ataishi chini ya masharti magumu mpaka kifungo chake kitakapomalizika mwaka 2029.

Kwa sheria za Afrika Kusini, wahalifu wote wana haki ya kuachiwa huru kwa msamaha mara tu watakapokuwa wametumikia nusu ya kifungo chao.

Pistorius aliingia gerezani Oktoba, mwaka 2014, alipohukumiwa kwa mara ya kwanza.

Miguu yake ya chini ilikatwa alipokuwa chini ya umri wa mwaka mmoja.

Baadaye Pistorius alitegemea viungo bandia na akawa mwanariadha mashuhuri duniani anayejulikana kama "blade runner."


Alikuwa na mafanikio katika Michezo ya Olimpiki ya Walemavu, akishinda medali nyingi za dhahabu, na akaimarisha sifa yake baada ya kushindana na wanariadha wasio na ulemavu kwenye Michezo ya Olimpiki ya London mwaka, 2012.

Idara ya huduma za kurekebisha tabia Afrika Kusini ilisema licha ya umaarufu wa nyota huyo wa zamani atachukuliwa kama mtu mwingine yeyote.

Hii ina maana atafungiwa nyumbani kwake kwa saa fulani za mchana na atapigwa marufuku kunywa pombe, pia hataruhusiwa kuzungumza na vyombo vya habari.

## HABARI MICHEZO

# UNITED YATARAJIA MARTIAL KUONDOKA



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inatarajia, Anthony Martial, ataondoka msimu wa joto unaokuja, licha ya pendekezo kutoka kwa Kocha, Erik ten Hag, kuhusu mazungumzo yanayoendelea juu ya mkataba mpya, kwa mujibu wa ESPN.

Ten Hag alithibitisha katika mkutano na wanahabari juzi United haijaanzisha nyongeza ya mkataba wa Martial ambao ungemweka Old Trafford hadi Juni, mwakani.

Mholanzi huyo alisema klabu hiyo "inazungumza" na Martial na wawakilishi wake lakini ESPN imesema majadiliano hayo hayana uwezekano wa kusababisha mkataba mpya.

Na sasa Mfaransa huyo ataondoka kwa uhamisho wa bure msimu wa joto unaokuja.

Martial ametumia miaka nane na nusu pale United baada ya kutoka Monaco mwaka 2015, akifunga mabao 90 katika michezo 317.

Hakucheza mwezi uliopita kwa sababu ya ugonjwa na kabla ya mechi ya tatu ya Kombe la FA dhidi ya Wigan Athletic hapo Jumatatu, Ten Hag alisema hatarajii mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kuwapo katika mchezo huo.

Ten Hag alithibitisha United imeanzisha nyongeza ya mwaka mmoja kwa Aaron Wan-Bissaka na Victor Lindelöf ambayo itawaweka wawili hao chini ya mkataba mpya hadi 2025.

Klabu imeamua dhidi ya kuanzisha chaguo kama hilo kwa Raphaël Varane, lakini iko tayari kuongeza mkataba wa beki huyo kwa masharti yaliyopunguzwa.

Varane atamaliza mkataba wake Juni na amekuwa huru kufanya mazungumzo na klabu nyingine kuanzia Januari Mosi, mwaka huu.

Wakati huo huo, United inakaribia kumtoa kwa mkopo, Jadon Sancho kwa klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund.

Timu hiyo ya Ujerumani inatazamiwa kulipa ada ndogo ya mkopo na kutoa mchango kwa mshahara wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.

"Siwezi kusema chochote kuhusu hilo," Ten Hag alisema hayo juzi.

"Inabidi tusubiri tuone jinsi mambo yanavyokwenda. Tukiwa na habari tutawaambia. Siwezi kusema lolote kuhusu suala hili kwa sababu hakuna habari."

# Barca inastahili heshima – Xavi

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernández alitoa wito wa "heshima kwa mabingwa watetezi" wakati kikosi chake kilitoka nyuma na kuilaza Las Palmas 2-1 na sasa imepitwa pointi saba na vinara wa LaLiga, Real Madrid na Girona.

Ilkay Gündoğan alifunga penalti ya dakika za lala salama na kuhitimisha ushindi huo baada ya Ferran Torres kufuta bao la kwanza la mshambuliaji wa zamani wa Barca, Munir El Haddadi, kwa Las Palmas kwenye Uwanja wa Gran Canaria.

"Bila shaka," alisema Xavi katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo alipoulizwa kama Barca bado walikuwa kwenye mbio za ubingwa.

"Uliona mechi za wiki hii kwenye LaLiga? Ni ngumu kwa kila mtu kushinda katika ligi hii.

"Girona ilishinda dakika ya mwisho, Madrid dakika ya 80 kwa mpira wa kona na sisi dakika ya mwisho kwa penalti. Kuna hoja kwa Barca kushinda LaLiga, ya kwanza ni sisi ndio mabingwa watetezi, hivyo heshima kwa mabingwa wanaotawala."

"Kama ingekuwa pointi 10, ingekuwa vigumu zaidi kushinda ligi, bila shaka, lakini mara zote unakuwa hasi," alisema Xavi alipoulizwa juu ya uwezekano wa kuanguka nyuma zaidi ya wale walio mbele.

"Inanifanya nicheke. Wewe sio sawa na makocha wengine. Tumeshinda mchezo kwa nini uulize swali hilo? Kwa nini kuzungumza juu ya kile ambacho hakikufanyika? Inaonekana kwangu ni upuuzi kabisa."

Ushindi huo uliathiriwa kidogo na jeraha la mapema kwa João Cancelo, ingawa Xavi ana matumaini hatampoteza beki huyo kulia kwa muda mrefu.

"Yuko sawa, kwa nadharia ni goti lake," alisema bosi huyo wa Barca akielezea hali ya Cancelo.



# Chicharito aamua kurejea Chivas




**MEXICO CITY,** Mexico

MSHAMBULIAJI wa zamani wa LA Galaxy na Mexico, Javier "Chicharito" Hernandez ametoa mwanga wa kijani kurejea Chivas, vyanzo vilimwambia Sergio Dipp wa ESPN.

Hernandez alimwambia Rais wa Chivas, Amaury Vergara, yuko tayari kucheza Liga MX 2024 Clausura katika klabu hiyo ambapo alianza kuichezea mwaka 2006.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 35 alikuwa na ofa kutoka Ligi Kuu ya Soka ya Marekani ( MLS), Ulaya na Mashariki ya Kati, lakini hakuna iliyovutia kama kurejea Guadalajara, ambapo sasa inaweza kuanza mazungumzo na uwakilishi wa mchezaji huyo.

Hernandez, mchezaji huru, kwa sasa anaimarika kikamilifu baada ya kupata jeraha la mwisho akiwa na LA Galaxy Juni, mwaka jana.

Baada ya mechi 82 na kufunga 39 katika misimu minne, na tuzo ya All-Star ya 2022 ya MLS, klabu hiyo ya MLS iliachana na mchezaji huyo.

Kabla ya jeraha lake na hatimaye kuondoka LA Galaxy, kiwango cha Hernandez kilianza kupungua mnamo 2023 akiwa na bao moja pekee katika mechi 12 katika mashindano yote.

Kabla ya kushika vichwa vya habari na kuhamia MLS mnamo 2020 - na kabla ya mbio zake kuu za Ulaya ambazo zilimfanya kutwaa mataji na kucheza akiwa na Manchester United, Real Madrid, Bayer Leverkusen, West Ham United na Sevilla, Hernandez alijipatia jina kwa mara ya kwanza akiwa na Chivas ya nyumbani kwao.

Licha ya kuwa mfungaji bora wa muda wote wa timu ya taifa ya wanaume ya Mexico, Hernandez bado hajaichezea timu hiyo tangu 2019.

Mshambuliaji huyo hajakataa kurejea katika timu ya taifa na alisema mwaka 2023 alizungumza na kocha wa zamani wa Mexico, Diego Cocca, kuhusu mlango uliobakia wazi kwa ajili ya kuitwa siku zijazo.

Chivas, kikosi cha pili kwa mafanikio zaidi cha Liga MX, kilikuwa nafasi ya tano katika msimu wa Apertura wa 2023.

HABARI MICHEZO

# SAMATTA AFUNGUKA LOLOTE LINAWEZA KUTOKEA AFCON

**Na Saada Akida**

NAHODHA wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta, amesema lengo la timu hiyo ni kupambana na kuhakikisha wanafanya vizuri katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023), zitakazofanyika kuanzia Januari 13 hadi Februari 11, mwaka huu nchini Ivory Coast.

Samatta alijiunga na kikosi cha timu hiyo kilichopo Misri juzi na kusema njia pekee ya kufikia malengo ni kuendelea kujiandaa vyema na si vinginevyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Samatta, alisema anaimani mwaka huu Taifa Stars itakwenda kushindana kutokana na kuundwa na kikosi imara zaidi.

**Straika huyo alisema kundi ambalo Stars imepangwa si jepesi kwa sababu ya historia ya wapinzani ambao wako nao katika kundi moja.**

"Kundi sio jepesi sana, niliwahi kusema lazima tuheshimu wapinzani wetu, tunahitaji kufanya vizuri hatua ya makundi na lazima tupambane, ndio njia pekee ya kufanikiwa, kwa kushinda mechi zetu zote," alisema Samatta.

Aliongeza anaamini kila mchezaji aliyeitwa akipata nafasi ya kucheza atakuwa na msaada mkubwa kwa timu ili kuhakikisha wanafanikiwa katika mikakati ya kusaka ushindi.

"Kinachotupeleka ni kwenda kushindana, tukijiandaa vizuri, naamini tutaenda kuwapa changamoto tuliokuwa nao katika kundi letu. Kundi letu ukiliangalia, sio kundi jepesi, lazima tuheshimu zile 'pot' wakati timu zinapangwa," Samatta aliongeza.

Naye Haji Mnoga, alisema yuko tayari kupambana na kusaidia Stars ifanye vyema katika fainali hizi.

"Tuko katika hali nzuri, tukishirikiana na tukipambana tutapata matokeo bora, nina furaha kuwa sehemu ya kikosi katika mashindano haya,

Stars itaanza kutupa karata yake ya kwanza Januari 17, mwaka huu kwa kuvaana na Morocco halafu itakutana na Zambia Januari 21 na itamaliza hatua ya makundi kwa kupambana na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).



Winga wa Azam FC, Iddi Suleiman 'Nado' akifanya mazoezi kuelekea mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayoendelea Visiwani Zanzibar. **PICHA: MTANDAO**

# JKT yawatisha Simba Queens

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Maafande wa JKT Queens ya Dar es Salaam wamesema hakuna timu yoyote yenye uwezo wa kuwazuia kutetea taji hilo wanalolishikilia, imeelezwa.

JKT Queens ndio vinara wa ligi hiyo na sasa inajiandaa kuikaribisha Simba Queens katika mechi ya raundi ya nne itakayochezwa Januari 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa JKT Queens, Masau Bwire, alisema wana kikosi chenye ubora mkubwa na wameshawaangalia wapinzani wao, hivyo wanaamini hakuna timu itakayovuna pointi kwao.

Bwire alisema ushindani uliopo katika ligi hiyo kwao si tatizo na wamejipanga kuchukua pointi tatu kwa kila timu watakayocheza nayo.

"Hatuhitaji kupoteza mchezo wowote msimu huu, tunafahamu ushindani na ugumu wa ligi, mechi yetu ijayo dhidi ya Simba Queens tunataka kuonyesha ubora wetu na JKT Queens nani katika soka la Tanzania, sisi wa kufananishwa na Mamelodi Sundowns Ladies na Al Ahly kwa wanawake," alisema Bwire.

Aliongeza wanajipanga kuendelea kutoa vichapo zaidi baada ya mechi iliyopita kupata ushindi mnono wa mabao 10-0 dhidi ya Amani Queens kutoka Lindi.

## Engola asajiliwa rasmi Msimbazi

INATOKA UK 24

Algeria.

Nyota wengine ambao wanatajwa kutua Simba katika dirisha dogo la usajili ni pamoja na kiungo wa Prisons, Edwin Balua na Ladak Chasambi kutoka Mtibwa Sugar.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, ameliambia gazeti hili kwa sasa akili yao ipo katika kutwaa Kombe la Mapinduzi lakini mchakato wa usajili utakapokamilika watawatangaza wachezaji wao wapya.

"Tunaweza kuwatangaza wachezaji wetu wapya kuanzia wiki ijayo, siyo kama tupo kimya usajili unaendelea, kilichopo ni hatujawatangaza tu," alisema Ahmed.

Aliongeza uamuzi wa wachezaji wapya wanaosajiliwa na watakaoachwa uko chini ya Benchikha kwa sababu ndiye aliyekabidhiwa dhamana hiyo.

"Usajili mkubwa unaendelea kufanyika usiopungua wachezaji watatu, mashabiki wa Simba wanatakiwa kuwa na subira kwa sababu viongozi wanafanya mchakato wa usajili kulingana na mahitaji ya benchi la ufundi na tuseme tunatarajia kushusha vifaa vipya," Ahmed aliongeza.

Benchikha na kikosi chake tayari wamefuzu hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yatamalizika ifikapo Januari 13, mwaka huu kwa bingwa kupata kitita cha Sh. milioni 100.

## Okrah apeleka hofu Yanga SC Mapinduzi Cup

INATOKA UK 24

kikosi cha kwanza, sasa nilitegemea na yeye ataongeza nguvu katika timu kuelekea michezo iliyoko mbele yetu," alisema Gamondi.

Aliongeza hatua wanayokwenda sasa katika mashindano hayo ni ngumu kwa sababu ukifungwa mchezo mmoja unatupwa nje ya mashindano.

"Tunaenda kwenye hatua ya mtoano, hii ni hatua ambayo hatupaswi kufanya makosa, tunahitaji kuwa imara na tayari kwa mapambano, hatuna muda mrefu wa kupumzika hivyo lazima tujipange vizuri," alisema Gamondi na kuongeza;

"Kwa wachezaji niliona katika mashindano haya nafurahishwa kwa namna wanavyojituma, kwa wachezaji vijana ambao wañapata nafasi ya kucheza wataonyesha uwezo mkubwa na katika kila mechi wanaimarika zaidi, michuano hii si tu tunataka ubingwa, lakini pia ni kwa ajili ya kuwapa nafasi vijana na wale ambao wamekuwa hawapati namba mara kwa mara katika kikosi cha Kwanza," alisema Gamondi.

Yanga imemaliza hatua ya makundi ikiwa na pointi saba, imeshinda mechi mbili dhidi ya Chipukizi na Jamus kutoka Sudan Kusini na juzi ililazimishwa suluhu na KVZ ambayo pia imetinga hatua ya robo fainali.

# Michezo



Jumamosi Januari 6, 2024
Nipashe

United yatarajia Martial kuondoka UK. 22



Kiungo wa Yanga, Jonas Mkude (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa KVZ katika mechi ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi iliyochezwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar jana usiku. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: MTANDAO**

## Okrah apeleka hofu Yanga SC Mapinduzi Cup

**Na Faustine Feliciane,**
ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameingiwa na hofu kufuatia winga mpya wa timu hiyo, Agustino Okrah, kuumia katika mechi ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya KVZ iliyochezwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex Visiwani hapa juzi.

Mechi hiyo ilimalizika kwa kila timu kushindwa kutikisa nyavu za mpinzani wake.

Katika mchezo huo, Okrah aliyeingia kipindi cha pili, aligongana na mchezaji wa KVZ wakati wakiwania mpira wa juu na kupeleka kupasuka chini kidogo ya paji la uso, na kulazimika kukimbizwa hospitali.

Gamondi aliliambia gazeti hili Okrah ame-kuwa katika mipango yake kuelekea mechi zilizobakia za michuano hiyo kutokana na kukosa wachezaji wake wa kikosi cha kwanza ambao wapo kwenye majukumu ya Timu za Taifa.

Kocha huyo alisema anafuatilia kufahamu ukubwa wa tatizo la winga hiyo waliyemsajili katika dirisha dogo la usajili lililofunguliwa na kujipanga upya.

"Aliumia vibaya, alipasuka kwenye paji la uso na kuanza kutoka damu puani, alipatiwa huduma ya kwanza na kutembea mwenyewe lakini alipelekwa hospitali, tunasubiri ripoti ya madaktari.

Ni mchezaji muhimu hasa katika mashindano haya, unajua sina wachezaji wengi wa

INAENDELEA UK 23

# Engola asajiliwa rasmi Msimbazi

## ●●● Yatajwa pia iko katika hatua za mwisho kumnasa Mzimbabwe Charamba...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WEKUNDU wa Msimbazi wameendelea kuimarisha kikosi chao kwa kukamilisha mazungumzo ya kumsajili beki wa zamani wa La Galaxy II ya Marekani, Jean Engola, raia wa Cameroon ili kuhakikisha wanafanya vizuri katika Ligi Kuu Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika, imefahamika.

Usajili wa Engola umekuja siku chache baada ya Simba kumtangaza kiungo mpya mshambuliaji kutoka JKU ya Zanzibar, Saleh Karabaka, ambaye amepewa mkataba wa miaka mitatu.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam zinasema Mcameroon huyo amefikia makubaliano ya kujiunga na Simba baada ya kuvunja mkataba wake na JKU ambayo ameitumikia tangu Agosti mwaka jana akitokea La Galaxy II.

"Mwalimu (Abdelhak Benchikha)amevutiwa na Engola na aliwasilisha jina kwa uongozi ambao sehemu kubwa umeshakamilisha mazungumzo na kinachosubiriwa ni kumtangaza rasmi kwa sababu tayari ameshavunja mkataba wake na JKU. Na JKU pia wameshaweka wazi kuachana naye.

Kocha amemwona hapa katika Kombe la Mapinduzi, amevutiwa na uwezo wake lakini hata ukiangalia wasifu wake wa kucheza La Galaxy imechangia kwa kiasi kikubwa kwa sababu ana uzoefu wa kutosha na maarifa mengi kutokana na alipopita, sijui mkataba wake ni wa muda gani lakini tayari wameshakamilisha," kilisema chanzo chetu.

**Taarifa zaidi zinasema Simba imemshusha straika mpya, Michael Charamba kutoka Chicken Inn ya Zimbabwe lakini pia wapo katika hatua za mwisho za mazungumzo na kiungo mkabaji wa Ittihad Tanger ya Morocco, Madicke Kane ili kuziba eneo Benchikha ameweka wazi lina changamoto.**

Kiliendelea kusema Benchikha anapanga kumaliza tatizo la Simba kukosa kiungo mkabaji asilia baada ya nyota waliopo kuonekana ni viungo wanaosaidia kukaba na kwenda kusaidia pia mashambulizi mbele, maarufu kama namba nane.

"Kuna mchezaji anaitwa Madicke Kane, huyu ni raia wa Senegal anacheza soka la kulipwa Morocco, tuko katika hatua za mwisho kama mambo yataenda vyema na yeye anaweza kushuka nchini siku za karibuni kwa sababu kipindi cha dirisha dogo la usajili kinakaribia kufungwa, tunataka kufanya haraka, ili wachezaji wote wajumuike mapema kuanza mazoezi ya pamoja," chanzo chetu kilisema.

Kiliongeza Benchikha anaamini ujio wa nyota hao wapya utafanya kikosi chake kiwe imara huku viungo waliopo sasa ambao ni Fabrice Ngoma, Mzamiru Yassin na Sadio Kanoute awatumie kama namba nane kutokana na asili yao si viungo wakabaji.

"Kocha kasema hawa waliopo atawapa majukumu mengine, na kasema Ngoma anaweza kucheza hata namba 10, ile namba anayocheza Chama (Clatous), jinsi anavyomwona aina ya uchezaji wake," kilisema chanzo hicho.

Awali ilielezwa Simba imeshamalizana na kiungo mkabaji, Erick Mbangossoum, anayeichezea Union Touarga ya Morocco, nyota hao wote pia wakiwa ni mapendekezo ya mwalimu huyo raia wa

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >